
TAIFA LEO
A NATION MEDIA GROUP PUBLICATION



## » Atoa kanuni za kufunguliwa kwa hoteli

HABARI UK 2

› Balozi wa Amerika akejeli Gavana kuhusu vifaa vya matibabu - UK 2

Jumanne, Aprili 28, 2020 · KSh30 · TSh500 · RFr300 taifaleo.nation.co.ke No. 20571

Naibu Rais akosa kushirikishwa kwenye mipango kukabili janga, ashindwa kutangamana na washirika

# CORONA YAONGEZA UPWEKE WA RUTO



Na WANDERI KAMAU

MASHARTI makali yaliyotangazwa na Wizara ya Afya kudhibiti kuenea kwa virusi hatari vya Corona yanaendelea kumzidishia upweke Naibu Rais William Ruto ambaye masaibu yake ya kisiasa yanaendelea kuongezeka kila uchao.

Dkt Ruto amekuwa akijikakamua pakubwa kuonyesha angali ngangari licha ya misukosuko inayokumba

ENDELEA Uk 2



Afisa Mkuu Mtendaji wa Hospitali Kuu ya Kenyatta Evanson Kamuri kwenye picha ya awali. *Picha/MAKTABA*

## Mkuu wa KNH akabwa koo kuhusu Walibora

SAMWEL OWINO Na CHARLES WASONGA

Hospitali Kuu ya Kenyatta imejitetea vikali dhidi ya shutuma kwamba, ilimtelekeza mwandishi mashuhuri Ken Walibora alipopelekwa huku kwa matibabu baada ya kupata ajali wiki mbili zilizopita.

Afisa Mkuu Mtendaji wa hospitali hiyo, Dkt Evanson Kamuri, alikanusha madai kuwa, wahudumu wake walimpuuza mwandishi huyo mahiri na mwanahabari alipofikishwa huko kwa matibabu Aprili 10.

Dkt Kamuri jana aliwaelezea wanachama wa Kamati ya Seneti kuhusu Afya hatua kwa hatua jinsi Profesa Walibora alipoteza maisha yake katika hospitali hiyo huku madaktari wakijizatiti kadri wawezavyo kumnusuru.

HABARI KAMILI Uk 3

### VIDOKEZO

**Tambiko la wazee kumaliza Corona** UK 4



**Kafyu yazima uhalifu kwa asilimia 50** UK 2

**CORONA ALIYELALA SELI AGEUKA MTETEZI SUGU WA MASKI** UK 4

Nation Media Group "Digital Copy"

# Balozi amkejeli gavana kuhusu vifaa

**Na LEONARD ONYANGO**

BALOZI wa Amerika humu nchini Kyle McCarter amemkejeli Gavana wa Kericho Paul Chepkwony kwa kuzindua tena vifaa vya matibabu vilivyokuwa vimezinduliwa miezi mitatu iliyopita.

Gavana Chepkwony wikendi alisambaza picha akiwa katika Taasisi ya Utafiti ya Walter Reed mjini Kericho, ambayo hushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Matibabu (Kemri) akisema vifaa hivyo vitatumika kupima watu 2,000 virusi vya corona kwa siku.

Taasisi ya Walter Reed hufadhiliwa na Serikali ya Amerika. Lakini Balozi McCarter alitia picha nyingine ya awali katika mtandao ya Twitter akisema kuwa: "Unarejelea vifaa hivi vilivyonunuliwa na Amerika na kuzinduliwa mnamo Januari 30, mwaka huu?"

Prof Chepkwony alijitetea kuwa taarifa yake ilisema wazi amezindua shughuli ya kupima virusi vya corona wala hakumaanisha alizindua vifaa vilivyokuwemo.

"Ndivyo hivyo (vifaa), tunashukuru Amerika," akasema Gavana.

Lakini Wakenya wengi waliofuatilia mdahalo huo walitilia shaka maelezo yake, wakauliza kwa nini hakusema kwenye taarifa yake kwamba vifaa vya kufanya uchunguzi wa kimatibabu vilikuwa vimeletwa Januari na Amerika. Prof Chepkwony alisema kuwa kaunti hiyo imekuwa ikituma sampuli katika Kaunti za Kisumu na Nairobi kufanyiwa vipimo vya corona.

"Maabara ya Kemri iliyoko Kericho imekuwa ikiboresha mashine zake za kupima virusi vya corona. Maabara hiyo sasa imethibitishwa kuwa imetimiza viwango vya kimataifa," akasema Gavana Chepkwony.

Kiongozi huyo wa kaunti alisema kuwa vifaa zaidi vya kupima virusi vya corona vitapelekwa katika maabara hiyo ili kuhakikisha kuwa sampuli za watu 6,000 zinapimwa kwa siku.

"Kufikia sasa watu waliopimwa katika Kaunti ya Kericho hakuna aliyepatikana na virusi vya corona," akasema. Wakati huo huo, shirika la Brighter Communities Worldwide la nchini Ireland limefungua wadi ya vitanda saba ya kutenga waathiriwa wa virusi vya corona katika hospitali ya Dubusat iliyoko katika eneobunge la Kipkelion Magharibi.

## Naibu Rais akosekana kwenye kampeni ya kudhibiti Corona, akosa kutangamana na wafuasi

# Ruto ajipata pweke kwake

KUTOKA Uk 1

Chama cha Jubilee, ishara kuwa ametengwa katika shughuli muhimu za serikali kuu. Na sasa, janga la corona limeonekana kuvuruga mipango yake kisiasa.

Mnamo wikendi, hali halisi ya upweke wake ilidhihirika kwa namna ambayo aliendeleza ibada ya Jumapili nyumbani kwake.

Kabla ya ibada za makanisa kusimamishwa nchini mwezi uliopita kutokana na tishio la janga la Corona, Dkt Ruto alikuwa kipenzi cha viongozi wengi wa makanisa, wakipigania kumwalika kwenye michango yao.

Wanasiasa wengi, hasa wa mrengo wa 'Tangatanga' walikuwa wakiandamana naye kwenye makanisa hayo, huku wakitumia majukwaa waliyopewa kuujibu Upinzani na yeyote waliyehisi "anamwingilia" Dkt Ruto.

Lakini Jumapili, ilibainika siku hizi analazimika kuandaa ibada na familia yake pekee kwenye chumba maalum cha maombi kilicho katika makao yake rasmi mtaa wa Karen, jijini Nairobi.

Kwenye picha alizoweka kwenye ukurasa wake wa Facebook, Dkt Ruto alikuwa na mkewe, Bi Rachael Ruto na watoto wao sita pekee huku chumba kizima kikiwa na viti tupu. Yeye na mkewe ndio walioongoza ibada.

Hili ni kinyume na ibada alizohudhuria, alikoalikwa na kupokelewa kwa shangwe na maelfu ya watu.

Na kama ishara ya kujiliwaza kutokana na hali inayomkabili, alinukuu kitabu cha Zaburi 27: 1-4 kwenye Biblia: "...wakati mahasidi wangu wanaungana kunimaliza, wao ndio watakaoangamia. Ingawa jeshi linaweza kuungana dhidi yangu, sitaogopa. Hata ikiwa vita vitaelekezwa kwangu, nitaendelea kuamini."

Katika Chama cha Jubilee, Naibu Rais angali anapigwa vita huku chama kiking'ang'aniwa kati ya upande wake na ule unaoegemea Rais Uhuru Kenyatta.

Dkt Ruto anapotikiswa na mawimbi ya kisiasa chamani ambapo anastahili kuwa na mamlaka makubwa kama naibu kiongozi, wandani wake wengi wamebaki kimya ikilinganishwa na awali.

Wengi wao wanasema wameamua kuendesha utetezi wao "kichinichini" kama vile kupitia mitandao ya kijamii, bila kutoa matamshi yoyote makali ilivyokuwa awali.

Wanadai kwamba si lazima waonekane wakimtetea hadharani, wakisisitiza kuwa "kuna njia nyingi."

Miongoni mwa wanasiasa walioenda chini ya maji ni aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Bw Mwangi Kiunjuri, wabunge Moses Kuria (Gatundu Kusini), Ndindi Nyoro (Kiharu), Kimani Ichung'wa (Kikuyu), Rigathi Gachagua (Mathira), Seneta Aaron Cheruiyot (Kericho) kati ya wengine.

"Vita vyetu vya kuikomboa Kenya bado vinaendelea. Hatutatikisika," alisema Mbunge wa Kiharu, Bw Ndindi Nyoro ambaye ni mmoja wa watetezi wakuu wa Dkt Ruto.

Kanuni za kuzuia watu kukongamana pia zimezima ziara nyingi za makundi ya kijamii na kidini ambazo zilikuwa zikifanywa nyumbani kwake Karen na Sugoi, Kaunti ya Uasin Gishu mara kwa mara.


Katika shughuli za kiserikali, Naibu Rais ameonekana kutengwa katika mikakati ya kupambana na janga la Corona hata ingawa anasisitiza wanawasiliana kila mara na Rais.

Rais hukutana na viongozi mbalimbali kupanga mikakati ya kupambana na corona wakiwemo magavana, lakini ni nadra sana Dkt Ruto kuandamana naye.

Hali hii imefanya juhudi za Tangatanga kueneza ajenda zao kwa ukakamavu kama zamani, wakati ambapo kuna madai kwamba Jubilee inapanga kuunda muungano na vyama vya ODM na KANU kwa maandalizi ya Uchaguzi Mkuu ujao.

Ili kutolea maoni habari hii, nenda kwa
taifaleo.nation.co.ke

**GHARIKA:** Mitaro yachimbika uwanjani



**MKAZI ajaribu kuvuka mtaro uliochimbika katika uwanja wa kandanda wa Shule ya Sekondari ya Liter, eneo la Elgeyo-Marakwet, kufuatia mvua kubwa iliyonyesha Jumapili. Mvua inayoendelea kunyesha imesababisha uharibifu usiomithilika huku familia nyingi zikipoteza makao na mifugo.** *Picha/Jared Nyataya*

# Serikali yatangaza kanuni mpya za kufungua mikahawa

**Na VALENTINE OBARA**

SERIKALI hatimaye imetangaza kanuni ambazo zitatumiwa kuruhusu mikahawa kuendeleza biashara zao bila kuweka wateja na wahudumu katika hatari ya kueneza virusi vya corona.

Kanuni hizo zilitangazwa jana na Waziri wa Afya, Bw Mutahi Kagwe, huku idadi ya waliopona ugonjwa wa Covid-19 ikipanda hadi watu 114.

Kufikia jana, idadi ya watu walioambukizwa pia iliongezeka hadi watu 363 baada ya watu wanane kupatikana wameambukizwa.

Miongoni mwa wanane hao, watatu walitoka Kaunti ya Mombasa, mmoja Kwale na wanne Nairobi.

Mikahawa mingi mijini ilifungwa wakati serikali iliposema watu wataruhusiwa tu kununua chakula cha kubeba ili kuzuia ueneaji wa virusi vya corona.

Katika masharti mapya, Bw Kagwe alisema ni lazima kila mhudumu athibitishwe hajaambukizwa corona kabla mkahawa ukubaliwe kuendelea na kazi.

Watu hawatakubaliwa kuingia wengi kwa wakati mmoja, na watakaoingia watahitajika kukaa mita moja unusu kutoka kwa wengine kila upande. Hakuna atakayeruhusiwa kutembeatembea ndani ya mkahawa isipokuwa wahudumu ambao watapelekea wateja vyakula mezani.

Vile vile, wateja lazima wanawe mikono kabla kuingia.

"Kama wahudumu watakuwa hawajapimwa corona, mkahawa wako hautafunguliwa. Masharti yote lazima yafuatwe," akasema katika kikao cha wanahabari Nairobi.

Ijapokuwa mikahawa itakuwa ikifunguliwa tu kati ya saa kumi na moja asubuhi hadi saa kumi jioni, wateja wataruhusiwa kununua pombe mkahawani.

"Pombe itauzwa pamoja na chakula ndani ya mkahawa na itakuwa kwa wateja wanaosubiri kupakuliwa chakula, wanaokula au dakika 30 baada ya mteja kumaliza kula," akasema Bw Kagwe.

# Kafyu imezima uhalifu kwa asilimia 50 -Serikali

**Na WANDERI KAMAU**

VISA vya uhalifu nchini vimepungua kwa asilimia 50 tangu serikali kuanza kutekeleza kafyu mwezi uliopita, amesema Katibu wa Wizara ya Usalama wa Ndani, Dkt Karanja Kibicho.


Hili ni kinyume na madai ya baadhi ya wananchi, kwamba sehemu kadhaa nchini zimekuwa zikikumbwa na ukosefu wa usalama hasa nyakati za usiku. Wengine pia wamekuwa wakiwalaumu polisi kwa kushiriki moja kwa moja kwenye uhalifu au kushirikiana na wahalifu kutekeleza maovu hayo.

Lakini kwenye mahojiano na kituo kimoja cha redio jana, Dkt Kibicho alisema kuwa kinyume na hayo, takwimu walizo nazo zinaonyesha kuwa visa hivyo vimepungua, hasa kutokana na utekelezaji wa kafyu.

"Takwimu tulizo nazo kuhusu hali ya uhalifu nchini zinaonyesha kuwa umepungua kwa asilimia hamsini kati ya Machi na Aprili mwaka huu. Hivyo, polisi hawapaswi kuelekezewa lawama kutokana na utovu wa nidhamu wa polisi mmoja," akasema.

Alieleza kuwa ni vigumu kwa wahalifu kuendesha maovu yao nyakati za usiku, ikizingatiwa kuwa baadhi ya maagizo ambayo maafisa wa usalama wamepewa ni kulinda mali ya wananchi.

Wiki iliyopita, baadhi ya wakazi wa Kitale, Kaunti ya Trans Nzoia, walilalamikia ongezeko la visa vya uhalifu, wakisema kuwa wahalifu wamekuwa wakivunja maduka yao licha ya uwepo wa maafisa wa usalama wanaopiga doria. Visa vya unywaji pombe haramu pia vimeripotiwa kuchipuka upya katika baadhi ya sehemu za Kati na mitaa duni ya jiji la Nairobi. Wakati huo huo, serikali imeonya kuwa huenda ikaongeza muda wa kafyu na marufuku ya kutotoka ama kuingia katika kaunti za Nairobi, Mombasa, Kilifi, Kwale na Mandera, ikiwa visa vya corona havitapungua.



**WAZIRI wa Usalama wa Ndani Fred Matiangi katika hafla iliyopita. Wizara yake imeripoti kupungua kwa visa vya uhalifu tangu amri ya kutotoka nje iwekwe.** *Picha/Maktaba*

## Uozo wa maadili ya vijana waendelea kuenea

UOZO wa maadili miongoni mwa vijana unaendelea kuenea, wakati ambapo taifa linajikakamua kupambana na virusi vya corona.

Vijana wengi wanapuuza masharti yanayolenga kuepusha ueneaji wa virusi hivyo wanapotenda vitendo vya usherati, huku maelfu wengine wakikusanyika katika mitandao ya kijamii kwa minajili hiyo hiyo.

Jana, polisi waliripoti kuwanasa watu 18 wenye umri wa kati ya miaka 14 na 30 katika mtaa wa Jamhuri jijini Nairobi mnamo Jumapili jioni wakiwa uchi wa mnyama.

Taarifa ya polisi wa kituo cha Kilimani ilisema kwamba waliarifiwa na umma kuhusu tukio lisilo la kawaida.

Maafisa walipoenda, walikuta watu hao wa kiume na wa kike, wakiwemo wanne wenye umri chini ya miaka 18 wakitengeneza video.

Wiki iliyopita, vijana 21 walikamatwa katika Kaunti ya Nakuru wakipiga picha za uchi. Naibu Kamishna wa Kaunti anayesimamia Nakuru Magharibi, Bw Elni Shafi, alisema vijana hao walinaswa baada ya wananchi kuarifu polisi.

*Hillary Kimuyu Na Valentine Obara*

**20684**

**Ukitaka kuwasiliana na 'Taifa Leo' tuma sms kwa nambari hii ukianza na neno Taifa.**

*Afisa mkuu asema madaktari walijizatiti vikali kuokoa maisha yake*

# KNH yajitetea kuhusu kifo cha msomi Walibora

SAMWEL OWINO Na CHARLES WASONGA


AFISA Mkuu Mtendaji wa Hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta (KNH), Dkt Evanson Kamuri, ametetea hospitali hiyo dhidi ya madai kuwa, wahudumu wake walimtelekeza mwandishi mahiri na mwanahabari Ken Walibora alipofikishwa huko kwa matibabu Aprili 10.

Dkt Kamuri jana aliwaelezea wanachama wa Kamati ya Seneti kuhusu Afya hatua kwa hatua jinsi Profesa Walibora alipoteza maisha yake katika hospitali hiyo huku madaktari wakijizatiti kadri wawezavyo kumnusuru.

"Madaktari wetu walijaribu kadri ya uwezo wao kuokoa maisha ya Profesa Walibora lakini kwa bahati mbaya alifariki," Dkt Kamuri akasema.

Kamati hiyo inayoongozwa na mwenyekiti wao, Seneta wa Trans Nzoia Michael Mbito, iliandaa mkutano ulioendeshwa kwa njia ya video ya Zoom.

Kulingana na Dkt Kamuri, Walibora alifikishwa katika KNH na ambulensi ya Serikali ya Kaunti ya Nairobi saa tatu na dakika 53 asubuhi, Aprili 10. Alitambuliwa kama Mwanamume Mwafrika asiyejulikana.



MWANDISHI Ken Walibora ambaye aliuawa kwenye ajali ya barabarani mapema mwezi huu.

**NAIROBI**

"Mgonjwa alikuwa akivuja damu na alikuwa na majeraha mabaya kichwani. Alihudumiwa katika kitengo cha wagonjwa waliojeruhiwa vibaya ambacho kina vifaa sawa na vilivyoko katika chumba cha wagonjwa mahututi (ICU)." Dkt Kamuri akasema.

Aliongeza kuwa, Profesa Walibora alikaa katika eneo hilo hadi saa kumi za jioni, akihudumiwa, kisha akawekwa katika chumba chenye mitambo ya kumsaidia kupumua.

Dkt Kamuri aliwaambia maseneta hao kwamba, hali ya marehemu Profesa Walibora ilikuwa mbaya zaidi mwendo wa saa mbili usiku kutokana majeraha aliyopata kichwa hali iliyomfanya kushindwa kupumua. "Lakini kwa mara nyingine, madaktari waliweza kumsaidia akapata uwezo wa kupumua," akaongeza.

Lakini ilipotimu saa sita na dakika 10 za usiku, Dkt Kamuri akasema, hali ya Walibora ilidhoofika zaidi kutokana hali kwamba, damu iliingia ubongoni mwake.

"Na mwendo wa saa saba na dakika 10, muda wa saa moja baadaye, tulimpoteza," akasema.

Dkt Kamuri alisema madaktari waliomhudumia Profesa Walibora kwa muda huo wote walikuwa; Dkt Rono, Dkt Sigilai na Dkt Okutoyi.

"Dkt Okutoti ni mtaalamu katika utabibu wa majeraha mabaya, na alisaidiana na wauguzi pamoja na wahudumu wengine wa afya ambao walikuwepo katia Hospitali kuu ya Kenyatta," akaeleza alipokuwa akijibu maswali kutoka kwa maseneta; Fred Outa (Kisumu) na Beth Mugo (Seneta Maalum).

Dkt Kamuri alisema kuwa hospitali ya KNH huwa haibagui wagonjwa na kwamba, ilimhudumia Walibora ipasavyo licha ya kwamba hakuwa ametambuliwa rasmi na hakuletwa huko na jamaa zake.

"Kwa hivyo, madai kwamba hospitali hii ilimtelekeza Profesa Walibora sio kweli hata kidogo," akasisitiza.

"Katika KNH, mgonjwa anapoletwa, huwa hatujali kama ana pesa au kadi ya NHIF au hadhi yako katika jamii. Kitu cha kwanza tunachofanya ni kutoa huduma za kwanza za kumtuliza mgonjwa kabla ya kuuliza malipo kwa sababu unaweza tu kulipa ukiwa hai," akaongeza.



**Bi Taifa**

**TERESIAH WAIRIMU**, 21. Yeye ni mzaliwa wa Elburgon katika kaunti ya Nakuru. Uraibu wake ni kusafiri, kusoma na kuogelea.

*Picha/John Njoroge*

## MUULIZE MJUAJI KOMBO

Kombo, nisaidie. Mchumba wangu hataki tukaribiane.
Kevo, Embakasi



Anatii mwito wa Serikali wa kuweka social distance. Huu ni msimu wa Corona

**SMS SWALI KWA NAMBARI YA SIMU 21603 UKIANZA NA NENO KOMBO**

**LAMU**

## Madiwani wataka wakazi wote Lamu wapimwe virusi vya corona

**MADIWANI** katika Kaunti ya Lamu wanataka wakazi wote wa Lamu wachunguzwe kimatibabu ili kufahamu hali yao ya virusi vya corona.

Madiwani hao, wakiongozwa na Kiongozi wa Wengi katika bunge la Kaunti ya Lamu, Bw Abdalla Baabad, walisema tayari wameanza mazungumzo na Gavana wa Lamu, Fahim Twaha na baraza lake la mawaziri ili kuanzisha kampeni maalum ya kuwapima kwa wingi wakazi katika kila wadi.

Lamu iko na jumla ya wadi 10, ambapo madiwani wanalenga kubuni vituo vya kupima maradhi ya Covid-19 katika kila moja ya wadi hizo.

Lamu ina jumla ya wakazi 143,920 kulingana na sensa iliyofanywa mnamo 2019.

Bw Baabad alisema ni vyema upimaji wa watu kwa wingi dhidi ya Covid-19 ufanywe haraka iwezekanavyo kwani idadi ya wakazi Lamu ni ndogo ikilinganishwa na kaunti zingine.

Aliwahimiza wakazi kujitokeza na kujua hali yao ya Covid-19 endapo vituo vya kupima vitabuniwa kwenye maeneo yao.

Pendekezo hilo limetolewa baada ya bunge hilo wiki jana kupitisha bajeti ya ziada ya Sh157 milioni ambazo zote zinalengwa kutumiwa katika vita dhidi ya Covid-19.

*Na Kalume Kazungu*

**NAIROBI**

## Waziri aendelea kukashifiwa kwa kuadhibu mtafiti mkuu wa KEMRI

**HATUA** ya Waziri wa Afya, Mutahi Kagwe kuagiza Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kimatibabu (Kemri) Dkt Joel Lutomiah ashushwe mamlaka, imeendelea kukashifiwa na Wakenya wa matabaka mbalimbali.

Mawakili, watafiti, wahadhiri na wanasiasa waliungana kukosoa hatua ya Bw Kagwe wakisema, haikufaa wakati huu na ni pigo kwa utafiti wa matibabu na dharau kwa wasomi nchini.

Bw Kagwe alimlaumu Dkt Lutomiah kwa kuchelewa kuwasilisha matokeo ya watu wanaopimwa virusi vya corona. Kulingana na Wizara ya Afya, Mnamo Aprili 15, Dkt Lutomiah alikosa kuwasilisha matokeo hayo kwa Bw Kagwe katika muda aliotakiwa kufanya hivyo ili yaweze kutangaziwa umma.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakili Nchini (LSK), Nelson Havi, alisema kwamba Dkt Lutomiah hakufanya kosa la kumfanya achukuliwe hatua.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Nairobi, Dkt Wandia Njoya alisema hatua ya Bw Kagwe ni dharau kwa wataalamu wa humu nchini.

*Na Benson Matheka*

Nation Media Group "Digital Copy"

NASAHA ya Ramadhan

# Kukabiliana na magonjwa ambukizi kwa mujibu wa Mtume SAW



Na KHAMIS MOHAMED

WAISLAM wanaendelea na ibada ya mfungo wa mwezi wa Ramadhan, huku ulimwengu ukiendelea kukumbwa na janga la virusi vya Corona. Janga lililoangamiza maelfu ya watu duniani, huku wengine wakiendelea kuhudumiwa katika hospitali mbalimbali.

Katika hali ya kukabiliana na ugonjwa huu wa kuenea waislamu hawaruhusiwi kukusanyika kwa ibada misikitini na hata kufanya mikusanyiko mikubwa ya kifamilia pamoja na marafiki wakati wa futari nyakati za jioni baada ya siku nzima ya mfungo, kama ilivyozoeleka.

Leo tungependa kuzingatia ushauri wa Mtume SAW kuhusu kukabiliana na magonjwa ambukizi kama hii ya Covid 19.

Kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba hivyo yafaa jamii kuchukua tahadhari za mapema kama vile kuosha mikono na kujiepusha kuzuru maeneo ambayo kuna maambukizi ya virusi vya Corona.

Uislamu umehimiza sana hatua ya kuchukua tahadhari huku ukifahamisha kwamba maradhi ya kuambukiza ni sehemu ya mitihani ya MwenyeziMungu kuwaonja waja wake ili iwe ni rehma kwa walio wema na adhabu kwa waja wake awatakao Allah (Swt).

Mama Aisha anasimulia kuwa alimuuliza Mtume SAW juu ya Tauni, Mtume SAW akamueleza kuwa *ilikuwa ni adhabu anayoipeleka Mwenyezi Mungu kwa mja amtakaye, na huyafanya Maradhi hayo kuwa ni rehma kwa Waumini. Basi hakuna mja atakayesibiwa na Tauni kisha akakaa ndani ya mji wake akisubiria na kutarajia malipo kwa Mola wake kwa kutambua kwamba hakuna litakalomfika ila lile ambalo MwenyeziMungu amemuandikia ispokuwa ujira wake ni kama wa Shahidi.* [Bukhari]

Ama kuhusu kuchukua tahadhari Mtume SAAW alisema:

*"Pindi mnaposikia mkurupuko wa maradhi ya tauni (Maradhi ya kuambukiza) msiingie katika mji huo uliokumbwa na maradhi hayo na yanapoingia maradhi hayo katika mji mnaoishi ndani yake basi msitoke".*

Hadithi hii ya Mtume Mtukufu alisema wakati ugonjwa wa kuambukiza kama huu wa COVID 19 unapoenea katika eneo, wakazi hawapaswi kuondoka eneo hilo na wengine hawapaswi kuingia katika eneo hilo kwani kufanya hivyo kutapelekea ugonjwa huo kuenea zaidi.

**RAMADHAN**
IWAPO UNA SWALI AU MAONI tutumie ujumbe unaoanza na neno SAUM kwa **20684**. Barua pepe: taifa@ke.nationmedia.com

## RATIBA YA LEO YA RAMADHANI

| MJI | KUFUNGUA | KUFUNGA |
|---|---|---|
| Nairobi | 6.33 | 5:15 |
| Mombasa | 6:19 | 5:08 |
| Kisumu | 6:42 | 5:23 |
| Kakamega | 6:43 | 5:23 |
| Eldoret | 6:41 | 5:22 |
| Garissa | 6:23 | 5:04 |
| Kitale | 6:48 | 5:18 |
| Mandera | 6:18 | 4:51 |
| Isiolo | 6:35 | 5:09 |
| Nyeri | 6:34 | 5:15 |
| Embu | 6:31 | 5:12 |
| Malindi | 6:20 | 5:07 |
| Lodwar | 6:35 | 5:12 |
| Lamu | 6:16 | 5:01 |

### Bw Obisa alikamatwa kwa kutovaa maski

# Aliyelala seli ageuka mtetezi sugu wa maski

Na WYCLIFFE NYABERI

**KISII**

MWANAMUME aliyekamatwa na kufungwa seli kwa kutovaa barakoa mjini Kisii, sasa amegeuka kuwa mwanaharakati wa kuhamasisha umma kuhusu umuhimu wa vitambaa hivyo vya kuzuia uenezaji virusi vya corona.

Bw Dennis Obisa, 33 alinyakwa na polisi mnamo Alhamisi iliyopita lakini akaachiliwa baada ya saa 16 ndani.

Alipokamatwa alikuwa akitoka kazini katika mtaa wa Mwembe, viungani mwa Kisii na alipofika sehemu za Gekomu-Menyinkwa, alipatana na polisi waliomtia mbaroni pamoja na watu wengine kisha wakapelekwa katika kituo cha polisi cha Kisii.

"Kwa hakika nilipata funzo nikiwa seli. Huko hali si nzuri. Kuna changamoto tele na singependa kuona vijana wenzangu wakipelekwa seli kwa kosa dogo kama kutovalia maski. Usiku wa manane nilipigwa na kibaridi kikali na mbu wakaning'ata kwa msiba wa kujitakia. Laiti ningalikuwa na barakoa ya Sh50, nisingalipigwa faini ya Sh5,000," akasema.

Mojawapo ya njia anazozitumia ili kufikisha ujumbe kwa watu ni kutumia mitandao ya kijamii hasa ule wa WhatsApp.

Njia hii imemfaa zaidi kwani ni ya haraka na hahitaji muda mwingi na kwa kuwa serikali imepiga marufuku watu kukongamana.

"Pindi tu nilipoachiliwa kutoka seli, watu wa kwanza kujua kilichonisibu ni wale wanaotumia WhatsApp. Siku za hivi karibuni nimekuwa nikihimiza watu kufuata maagizo yanayonuia kupunguza maenezi ya corona kwani ndilo janga linalozungumziwa kila pembe ya dunia," akasimulia.

Njia nyingine anayoitumia hasa kwa kina mama na watu wengine wakongwe ni kuwatembelea katika nyumba zao na kuwatahadharisha kuhusu ugonjwa huo.

Anapofika kwao yeye husisitiza umuhimu wa kunawa mikono mara kwa mara kwa kutumia sabuni na maji safi.

Amefaulu kuwatengenezea baadhi ya wakongwe ndoo za kubuni ili ziweze kupitisha maji kwa mtiririko mtu anaponawa kwa kupata maelezo kutoka kwa vyombo vya habari.

"Mimi hufuatilia kwa karibu yale tunayoelezwa na serikali kupitia redio na runinga na hata kwenye mtandao. Kwa kuwa watu wakongwe mara nyingi hawana uwezo wa kumiliki vyombo hivyo, ninawasaidia kuwafahamisha yale yanayoelezwa na kusisitizwa na wizara ya afya," akasema Bw Obisa.


"Pia ninapowakuta watu wakiwa wamesimama njiani, mimi huwaomba angalau dakika zao chache ili kuwafunza mawili matatu kuhusu virusi hivi. Wakati mwingine nakutana na vijana kwenye makundi wakiwa wamesimama barabarani bila kutimiza hitaji la umbali wa mita moja kutoka kwa mtu mwingine. Hapa nachukua jukumu la kuwaonyesha jinsi wanavyofaa kufanya endapo italazimu wakutane," akaeleza.

Alitoa wito wahisani wajitolee kusambazia umma barakoa za kutosha.

"Inasikitisha sana unapomwona mtu ametumia barakoa iliyokuwa ya kitambaa chaeupe lakini imegeuka rangi na kuwa kitu kingine. Hili linahatarisha hata zaidi maisha yao na ninaomba wahisani na viongozi wetu wajitokeze na kusaidia katika hili," akasema.

Zaidi ya yote, amewapa changamoto vijana wenzake kuiga mfano wake na kumuunga katika kampeni yake ya kuhamasisha wakazi ili kupiga vita virusi vya Corona. Lengo lake ni kuwafikia watu wengi ikiwa atapigwa jeki na watu wengine wenye nia nzuri kama yake.

**CORONA: HATUA ZA KUDHIBITI MAAMBUKIZI**




**DEREVA wa trela ahudumiwa katika Lango 24 eneo la Maegesho ya Magari la Mamlaka ya Bandari Nchini(KPA) ambapo hatua za kudhibiti coronavirus katika Bandari ya Mombasa zimechukuliwa kulinda wafanyakazi na umma kwa jumla dhidi ya maambukizi hayo. Wafanyakazi kadhaa wamelazimishwa kuwekwa katika karantini.** *Picha/Kevin Odit*

# Aliyeua mlinzi wa Gavana Kingi 'apata afueni'

Na PHILIP MUYANGA

**MOMBASA**

MSHUKIWA wa kundi la Mombasa Republican Council (MRC) ambaye alikuwa amehukumiwa kifo kwa kumuua aliyekuwa mlinzi wa Gavana wa Kilifi Amason Kingi miaka minane iliyopita alipata afueni baada ya hukumu hiyo kubadilishwa kuwa kifungo cha miaka 40.

Hata hivyo, Mahakama ya Rufaa ilitupilia mbali rufaa ya Bw Faraji Konde kuhusu kupatikana na hatia ya mauaji ikisema kuwa haikuwa na msingi wowote.

Majaji wa Mahakama ya Rufaa Daniel Musinga, Gatembu Kairu na Agnes Murgor walisema ijapokuwa mshtakiwa alijitetea kwamba yeye ni anayetegemewa katika familia, hakuonyesha dalili za kutubu makosa yake.

"Kutilia maanani kifo cha kinyama marehemu kilichomkumba, hukumu kali ya kukaa gerezani inafaa," majaji hao walisema.

Bw Konde alishtakiwa pamoja na watu wengine watatu kwa shtaka la mauaji ya konstebo wa polisi Harrison Maitha Mweni.

Kulingana na upande wa mashtaka, kitendo hicho kilitokea mnamo Oktoba 4, 2012 katika uwanja wa Mtomondoni, mjini Mtwapa kaunti ya Kilifi.

# Wazee Baringo wafanya tambiko kufukuza corona

Na SAMUEL BAYA

WAZEE wa jamii ya Tugen katika mpaka wa kaunti za Baringo na Nakuru mwishoni mwa juma walifanya maombi ya kitamaduni katika tambiko ambalo lililenga kukemea virusi vya corona.

Zoezi hilo lilifanyika katika kilele cha kilima cha Koisamo kuanzia mwendo wa saa nne asubuhi. Kilele chake kilikuwa ni kuchinjwa kwa beberu mweupe aliyenonona ili kutoa sadaka kwa Mungu.

Akiongea na Taifa Leo, mzee wa jamii hiyo Chemjor Chelagat anayetoka katika rika la Kipkoimet alisema wanamwomba Mungu aharakishe kuondoa janga la corona duniani. Walikuwa wamevaa barakoa na kuweka nafasi kati yao kama inavyotakikana na wizara ya afya.

Walitumia kinu maalum ambacho kiliwekwa kwa miti ya asili ambayo jamii hiyo inaamini kwamba ni ya kusaidia kufukuza jambo lolote baya.

Baadaye mbuzi alichinjwa na mmoja wa wazee hao akanywa damu yake kabla ya kuanza kuchomwa.

"Ule moshi unavyoelekea mawinguni, tunaamini kwamba utamfikia Mungu na maombi yetu yatasikika," akasema Mzee Chemjor.

Akiongea na Taifa Leo, Bw Samuel Moro kutoka rika la Kaplelach alisema kuwa maombi hayo ni muhimu.

"Huu ni mojawapo ya utamaduni ambao jamii zetu zimehifadhi kwa miaka na vikaka na mara nyingi maombi kama haya yanayoshirikisha utoaji wa sadaka yanatokana na jambo zito ambalo huwa linatupata kama jamii," akasema.

Alisema kuwa baada ya tambiko hilo, wanaamini kwamba mungu atafungua njia na kuweka mambo sawa na hatimaye ugonjwa wa Covid-19 utamalizika.

Bw Harry Cheruiyot ambaye ni miongoni mwa wale wazee ambao walipata elimu katika jamii hiyo alisema tukio hilo ni maombi ya utakaso sawa na yaliyotajwa katika vitabu vya dini.

Alisema hata katika vitabu vya dini imeandikwa kwamba zamani kulikuwa na hitaji la kutoa sadaka baada ya dhiki kukumba mataifa.


"Mimi nilizaliwa na kulelewa hapa na tukio hili ni la aina yake kuwahi kutokea. Ndio maana ninasema kwamba huu ni utamaduni muhimu sana. Maombi ni muhimu na mataifa hufanya hivyo wakati wa dhiki. Sisi kama jamii tunatambua umuhimu wa maombi na utakaso wa kiasili," akasema.

Nation Media Group "Digital Copy"




Nation Media Group "Digital Copy"

## KCPE SOCIAL STUDIES / CRE 2020 PAPER F




**Study the map of Zena area and answer questions 1-7**

1. The land of Zena area rises from
A) North West B) South West
C) North East D) South East

2. Zena town developed in the region mainly because?
A) The area has low temperature
B) There is a road junction
C) The area is densely populated
D) The area has adequate security

3. River Zena meanders as it flows northwards. This is mainly because?
A) The area is generally flat
B) The area is hilly
C) The area is on high altitude
D) The area has many economic activities

4. Which social service is not provided in Zena town?
A) Banking service B) Health service
C) Security service D) Education service

5. Three of the following statements are true about Zena area. Which one is not?
A) Zena area is a county
B) Pili sub-county receives low rainfall
C) Witu sub-county has black cotton soil
D) The main form of transport is road

6. Which economic activity is not carried out in Pili sub-county?
A) Livestock keeping B) Fishing
C) Trading D) Crop farming

7. The citizens of Pili sub-county were asked to suggest a development project to be established in their area. Which one would they suggest?
A) A police station B) A school
C) A cattle dip D) A healthy center

8. Three of the following statements are true about Buganda kingdom. Which one is not?
A) Kingship was hereditary
B) The king controlled trade
C) Omuanika was the title of chief justice
D) Bataka distributed the land

9. Who among the following homids did not walk upright?
A) Homo erectus B) Homo habilis
C) Homo sapien D) Homo sapien sapien

10. Conflicts among students in school can best be resolved through
A) Sending away disobedient students
B) Bringing back the cane in school
C) Transferring head teachers
D) Having students participate in decision making

11. Which group of early visitors to Eastern Africa came as administrators?
A) Said Seyyed,John Speke
B) British, Germans
C) H. M Stanley, Carl Peters
D) Dr.Krapf, David Livingstone

12. The revolution of the earth causes seasons due to
A) Changing in the position of the overhead sun
B) Difference in time along different longitudes
C) Rotation of earth on it's axis
D) Changes in the direction of wind

13. A nuclear family is made up of
A) Father, mother, adopted child
B) Father, uncle, cousin
C) Mother, sister, aunt
D) Mother, father, grandmother

14. Which group consists of River Lake Nilotes in Uganda?
A) Acholi, Karamajong, Iteso
B) Acholi, Langi, Alur
C) Acholi, Shilluk, Alur
D) Acholi, Langi, Nuer

15. Most towns along the coast of Eastern Africa developed mainly as a result of
A) Water transport B) Administrative activities
C) Trading activities D) Tourism activities

16. The best method of preserving fish in the deep sea is
A) Deep freezing B) Sun drying
C) Salting D) Smoking

**Use the diagram below to answer questions 17 and 18**




17. The diagram shown represents the formation of a
A) Convectional rainfall B) Sea breeze
C) Cyclonic rainfall D) Land breeze

18. The above condition occurs mainly during the
A) Hot season B) Day time
C) Cold season D) Night time

19. Which one of the following combination of factors will contribute to slow population growth rate?

| A | B |
|---|---|
| Improved medical care | Birth control measures |
| High mortality rate | High mortality rate |
| Cultural values | Late marriage |

| C | D |
|---|---|
| Improved nutrition | Spread of HIV/ AIDS |
| Improved education | Cultural values |
| Low fertility rate | Improved medical care |

20. Which one of the following statements is true about small scale farming in Kenya?
A) The yields are always low
B) Work is often done using machines
C) Some farmers keep livestock
D) The products are usually exported

21. In Kenya, a parliamentary bill becomes law only when it has been signed by the
A) Attorney General B) Chief Justice
C) President D) Speaker

22. Which one of the following is not a social right of a child?
A) Right to education
B) Right to good health
C) Right to play
D) Right to earn a living

23. In Bamburi limestone is mined using
A) Deep shaft method B) Open Cast method
C) Drilling method D) Underground method

24. One function of the council of elders among the Ameru during the pre-colonial period was to
A) Make laws B) Treat the sick
C) Carry out raids D) Foretell the future

25. Below are statements about an African leader in the pre-colonial period
i. He became a king and ruled from 1854-1884
ii. He welcomed the church missionary society and Roman Catholics in his territory
iii. He collaborated with the British as they established sphere of influence in Eastern Africa
The leader described above is
A) Kabaka Mwanga B) Laibon Lenana
C) Lewanika D) Kabaka Mutesa 1

26. Which one of the following physical features was formed as a result of down warping process?
A) Rift valley B) Lake Victoria
C) Bilesha plains D) Lorian swamp

27. Coastal tropical climate in Eastern Africa is best characterized by
A) It's low temperature and rainfall
B) It's high temperature and rainfall
C) It's low humidity and high rainfall
D) It's long rainy season


28. The most important affect of high relief in an area is that
A) It provide a good site for communication equipment
B) It is usually suitable for forests
C) It causes increase in temperature
D) It causes relief rainfall

29. Three of the following statements are true about desert climatic region of Eastern Africa. Which one is not?
A) The region receives very little rainfall
B) Rainfall is irregular
C) High temperature are experienced
D) It covers half of the surface area in Eastern Africa

30. Forest vegetation is mainly influenced by
A) Availability of high rainfall
B) Presence of fertile soil
C) Well drained slopes
D) Human activities such as construction

31. Below are characteristics of a type of vegetation found in Eastern Africa
i. Made up of open woodland
ii. Trees do not form canopies
iii. Grass grows on the surface
iv. Cover parts of Kenya and central Tanzania
The vegetation type described above is
A) Savannah grassland B) Desert vegetation
C) Miombo woodland D) Tropical rainforest

**Use the map below to answer questions 32-35**




32. The country marked P is headed by
A) A nominated prime minister
B) A hereditary king
C) An elected king
D) An elected president

33. The river marked H is
A) Orange B) Limpopo
C) Cunene D) Zambezi

34. The main economic activity practiced in the place marked S is
A) Mining B) Fishing
C) Crop farming D) Livestock keeping

35. Which community is likely to be found in the area marked W?
A) Xhosa B) Hausa
C) Bakongo D) Berbers

36. The Fulani pastoralists settle in the high Bauchi and Jos plateau because
A) It is safe from attacks
B) It is free from tsetse flies
C) It is rich in pasture
D) It has high rainfall

37. Sahel region in Africa is sparsely populated mainly because it
A) receives low rainfall
B) has poorly drained soil
C) experiences high temperature
D) has harmful pests

38. Below are benefits of interaction among communities except
A) Enrichment of culture
B) Promotion of trade
C) Contribution to population growth
D) Exchange of ideas hence faster development

39. The school routine is important because it
A) reduces the work of teachers on duty
B) forces everybody to fellow the program
C) ensures pupils go for break at the right time
D) ensures that planned activities run systematically and smoothly

40. Who writes minutes during a committee meeting in a public primary school?
A) Committee chairman B) Deputy head teacher
C) Committee treasurer D) Head teacher

41. The most basic unit in the society is the
A) Family B) Age-group
C) Clan D) Age-set

42. The government of Kenya is expanding the Standard Gauge Railway to many parts of the country mainly to

Nation Media Group "Digital Copy"

A) Fulfill its manifesto it promised during campaign
B) Promote trade through fast transport
C) Convince citizens to vote for it again
D) Enable many people to go to Mombasa

43.Which one of the following UN agencies standardizes world economic system?
A) FAO B) UNESCO
C) World Bank D) UNDP

44.One of the social functions of the commonwealth is to
A) promote parliamentary democracy among members
B) encourage trade among member countries
C) promotes educational exchange programs among members
D) send observers to member states during elections

45.Which one of the following organizations was formed to maintain close relationship between the former colonies and their master?
A) The United Nations B) The AU
C) The O.A.U D) The commonwealth

46.The road sign shown below can be found in the following areas except?




A) Near a town
B) On the highway
C) Near a school
D) Near a hospital

47. First Aid is given to a victim of accident mainly to
A) save life
B) treat the victim
C) bring the victim to life
D) demote recovery

48.The government promotes growing of flowers in the country mainly to
A) earn foreign exchange
B) create jobs for the youth
C) promote local industries
D) put idle land under utilization

49.Democracy in a country is best seen when
A) Citizens are forced to join political parties
B) Human rights are respected
C) Citizens are denied a chance to vote
D) The government create jobs for all

50. The imperial British East Africa Company (IBEA co) stopped administrating Kenya because
A) The company was abolished
B) White settlers opposed it
C) British government took over the administration
D) The company lacked funds

51. When Kenya was declared a republic the head of state assumed the little
A) Prime minister B) Chief Minister
C) President D) Governor

52.The British government built the Kenya – Uganda railway mainly to
A) make administration easy
B) to promote the spread of Christianity
C) transport goods to the coast
D) transport soldiers to the interior

53.One of the duties of African chiefs in Kenya during the colonial period was to
A) Conduct oathing ceremonies
B) Nominates people to the Native-councils
C) Provide security to freedom fighters
D) Organize for supply of labour to settler farms

54.A foreigner who wishes to become a Kenyan citizen is required to obtain
A) A registration certificate
B) A Kenyan ID card
C) A birth certificate
D) A marriage certificate

55.The main factor influencing the location of a furniture making industry is
A) Availability of power
B) Availability of market
C) Availability of raw materials
D) Availability of labour

56.The Atlas mountains were formed as a result of
A) Volcanicity B) Faulting
C) Folding D) Erosion

57. Rapid population growth in some parts of the rural Kenya has resulted to
A) Reduction of areas under forest
B) Increase in soil erosion
C) Inadequate water for domestic use
D) Shortage of land for industries

58.Who among the following officials is not a member of judiciary?
A) Chief justice B) Judges
C) Magistrates D) Attorney General

59.The main source of revenue for the National government is
A) Loans and grants
B) Sale of government bonds
C) Taxes
D) Sale of government property

60. Reconciliation refers to
A) taking our enemies to court
B) re-establishing good relations
C) obeying the law
D) leaving our enemies alone

## C.R.E

61. God created man and woman and placed them in the garden of Eden mainly to
A) Eat the fruits in the garden
B) Cultivate and take care of it
C) Name the animals in the garden
D) Make shrines and worship God there

62.Why did God tell Noah to build the Ark?
A) To save him and his family
B) To test Noah's obedience to Him
C) Noah had the skills to build the ark
D) God wanted Noah's family to be Holy

63.The outwards sign that Abraham and all his descendants had entered a covenant with God was
A) Rainbow B) Blood of Jesus
C) Circumcision D) Smoking firepot

64.The Jews celebrate their Passover feast to
A) Remember how they crossed Red sea
B) Remember how God provided them with manna
C) Remember how God killed all the Egyptian firstborns
D) Honour God for what He did for them

65.King Ahab sinned before God. Which two commandments did he break?
A) Coveting and idolatry
B) Murder and coveting
C) Adultery and murder
D) Idolatry and Adultery

66.Who advised Moses to choose judges to help him?
A) Jethro B) Caleb
C) Aaron D) Samuel

67. 'Turn away from your sins and be baptized and God will forgive your sins' (Mk 1:4). These words were said by
A) Jesus Christ B) Isaiah
C) Peter D) John the Baptist

68. After Jesus was tempted by the devil, he began his ministry in the province of
A) Bethlehem B) Jericho
C) Galilee D) Samaria

69.Which one of the following events took place during the transfiguration of Jesus?
A) The Holy Spirit come down in the form of dove
B) His clothes become dazzling white
C) There was a strong wind
D) Holy spirit came down inform of fire

70.All the following parables teach about prayer except one. Which one? The parable of
A) The Pharisee and the tax collector
B) The sower
C) The widow and the judge
D) The friend at night

71. Which one of the following miracles did Jesus perform after resurrection?
A) The miraculous catch of fish
B) Raising Jairus daughter
C) Changing water into wine
D) Raising son of widow of Nain

72. 'I see heaven opened and the son of man standing at the right side of God' (Acts 7:56). These words were spoken by
A) Stephen B) Saul
C) Jesus D) The injured man

73. At Ephesus believers received the Holy Spirit when Paul
A) Preached the word of God
B) Baptized them
C) Laid hands on them
D) Shared communion with them

74. The main reason why Jesus Christ choose the twelve disciples was to
A) Baptize people
B) Distribute food and funds to widows
C) Give him protection during his ministry
D) Build the church through them

75. 'It is kindness that I want not animal sacrifice. I have not come to call respectable people but outcasts.' When did Jesus use these words?
A) When raising Lazarus
B) When he visited Zachaeus home
C) When calling Matthew
D) When calling Philip

76. What did prophetess Anna say about the baby Jesus when he was presented in the temple? He
A) will be the light to the gentiles
B) will set Jerusalem free
C) will be called son of the Most High God
D) will be called Mighty God

77. The main teaching in the parable of the lost son is
A) Patience B) Forgiveness
C) Importance of prayers D) Thanksgiving

78. Jesus taught his disciples that when fasting they should
A) Not show people that they are fasting
B) Pray in faith
C) Do it in public places
D) Wear sack cloths

79. The men who brought a paralyzed man through the roof showed that
A) They knew Jesus
B) The paralyzed man was their friend
C) Other people were bringing sick people to Jesus
D) They had great faith in Jesus

80. Which promise of Jesus to his disciples was fulfilled fifty days after his resurrection?
A) Meeting his disciples in Galilee
B) Choosing of Mathias
C) Ascending to heaven
D) The coming of the Holy spirit

81. Which one of the following events happened when Jesus was on the cross?
A) A cloud covered Jesus
B) Two angels appeared
C) Darkness covered the whole world
D) Holy spirit came down inform of fire

82. The book of Acts mainly describes
A) The activities of Jesus Christ
B) How the good news was spread
C) The preaching of John the Baptist
D) Paul's letter to the early church

83.People in traditional African societies respected ancestors because
A) They link the living with God
B) They died a long time ago
C) They brought rain
D) The living are named after them

84. A common belief in both traditional African religion and Christianity is that
A) Jesus was the son of God
B) Creation is the work of God
C) There is the resurrection of the body
D) Death is caused by sin

85.'Are you the only visitor in Jerusalem who doesn't know the things that have been happening there the last few days? (LK 24:18) On which occasion were these words said
A) Ascension of Jesus
B) Resurrection of Jesus
C) Transfiguration of Jesus
D) Pentecost

86. The best way for a Christian pupil to promote good behavior in school is by
A) Praying for the school
B) Being a leader
C) Being obedient
D) Being a good model

87. In the traditional African society gifts were given to new born babies in order to
A) Appreciate them
B) Make them happy
C) Give them identity
D) Welcome them in the community

88. Expectant mothers wore amulets in the traditional African community in order to
A) Make them look beautiful
B) Identify them in the community
C) Enable them deliver successfully
D) Protect them from harm

89. The main value expected of young men after initiation was
A) Responsibility B) Patience
C) Tolerance D) Obedience

90 Which missionary translated the Bible to Kiswahili?
A) Johannes Rebmann B) Ludwig Krapf
C) David Livingstone D) Jacob Ehardt

## Kipengo




Nation Media Group "Digital Copy"

TAIFA LEO

NATION CENTRE KIMATHI STREET NAIROBI

# Tusilegeze kamba dhidi ya corona

HUKU Kenya ikionyesha dalili za kuanza kulegeza kanuni za kupambana na ueneaji virusi vya corona, inahitajika hamasisho ziendelee kutolewa kuhusu hatari ambayo ingali iko.

Kufikia sasa, hakuna dawa wala chanjo inayotambulika ambayo imepatikana kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19 kimataifa.

Majaribio ya dawa na chanjo ambayo yamefanywa kufikia sasa hayajaleta mafanikio.

Vile vile, wataalamu wanasema hata dawa au chanjo ikipatikana sasa, itachukua muda mrefu mno kabla iidhinishwe kutumiwa kwa binadamu. Haya yanadhihirisha kuwa safari ingali ndefu katika vita vya kukabiliana na virusi hivyo. Hatua ya serikali kutoa kanuni zitakazosimamia ufunguzi wa mikahawa ni kwa minajili ya kuanza kurudisha biashara ili kupunguza madhara ya kiuchumi.

Kufikia sasa, biashara nyingi tayari zimepata hasara kubwa tangu mgonjwa wa kwanza wa coronavirus alipotangazwa kupatikana Kenya. Hali hii imefanya maelfu ya watu kote nchini wamepoteza kazi zao na hawana namna ya kupata riziki. Hatua zimepigwa kwa kutibu wagonjwa wapatao 114 kati ya 363 walioambukizwa, lakini hatuwezi kusahau vifo 14 ambavyo vilitokea. Kimataifa, nchi nyingi zimeanza kulegeza kanuni za kuepusha ueneaji wa virusi hivyo ili kuanza kuokoa uchumi.

Hatua chache tulizopiga kufika sasa hazifai kurudishwa nyuma kwa hivyo chochote kile kinachofanywa, kifanywe kwa tahadhari kubwa.

Wamiliki wa mikahawa itakayofunguliwa ni sharti wahakikishe kutakuwa na nidhamu kikamilifu miongoni mwa wahudumu na wateja wao. Hatungependa kuwa kama nchi ambazo zilidhani zimeanza kupata ushindi kisha maambukizi yakaanza tena kuongezeka.

Wito huu si kwa mikahawa pekee, kwani imebainika pia majengo kadhaa ya kibiashara ambayo yalikuwa yamefungwa, sasa yameanza kufunguliwa.


Ni jukumu la wahusika wote katika biashara hizi kutambua kwamba kile watakachofanya kitaokoa au kuhatarisha maisha yao wenyewe, wala sio ya wateja wao pekee.

Haitakuwa busara kwa mtu yeyote kusubiri kufuatiliwa na serikali ndipo atekeleze mipango ya kuepusha maambukizi ya virusi vya corona katika nchi hii.

Watu wasitazame hatua ya serikali kuanza kulegeza masharti kama idhinisho la umma kuanza kulegeza kamba katika vita hivi.

Ni Gazeti la Kampuni ya Nation Media Group
**Mkurugenzi Mkuu: STEPHEN GITAGAMA**
**Mkurugenzi wa Uhariri: MUTUMA MATHIU**
**Mhariri : PETER NGARE**

# *Serikali sasa haina budi ila kuahirisha mitihani*



**WANAFUNZI wakiwa darasani.** *Picha/Maktaba*

**NA CHARLES WASONGA**

HATUA ya serikali ya kuongeza muda wa utekelezaji wa amri ya watu kutoingia na kutotoka kaunti za Nairobi, Mombasa, Kwale, Mandera na Kilifi kwa siku 21 zaidi pamoja na kafyu, imeongeza wasiwasi zaidi katika sekta ya elimu ya msingi.

Wiki iliyopita kumeibuka mjadala miongoni mwa wazazi, walimu, vyama vya kutetea masilahi ya walimu na serikali kuhusu iwapo mitihani ya kitaifa inapasa kuahirishwa au la.

Kuendelea kufungwa kwa kaunti tano nchini kwa siku siku 21 zaidi kutokana na ongezeko la maambukizi ya Covid-19, kunamaanisha kuwa kalenda ya masomo itaendelea kuvurugwa.

Ni wazi kuwa muhula wa pili ambao, kwa mujibu wa kalenda hiyo unapasa kuanza Mei 4, hautaanza kwa sababu siku ya mwisho ya marufuku hii ni Mei 16, 2020.

Huku ikionekana wazi kwamba hatua zinazotekelezwa kudhibiti corona zitavuruga maandalizi ya watahiniwa, serikali imesimama kidete kwamba mtihani wa kitaifa wa darasa la nane (KCPE) na ule wa kidato cha nne (KCSE) itaendelea ilivyopangwa.

Juzi, Waziri wa Elimu Profesa George Magoha alishikilia kuwa hamna haja ya kuahirishwa kwa mitahani hiyo.

Ajabu ni kwamba Rais Uhuru Kenyatta alionekana kuunga mkono kauli hiyo akisema mitihani hiyo haitasongezwa akisema serikali itatoa mwelekeo kuhusu jinsi wanafunzi wa darasa la nane na kidato cha nne watafidia muda waliopoteza.

Kwa kuwa idadi ya wanaoambukizwa Covid-19 inaendelea kuongezeka kila siku, uwezekano wa kupatikana haraka kwa chanjo ukiwa finyu, na serikali ikiendelea kutumia baadhi ya shule za upili za mabweni kama vituo vya karantini, Wizara ya Elimu inapasa kuahirisha mitihani ya kitaifa.

Kwanza, ni wazi kwamba ugonjwa huu ni hatari, na unawaua wakubwa kwa wadogo, hivyo sidhani kuna mzazi atakubali kuwarejesha watoto wake shuleni kabla ya janga hili kudhibitiwa.

Na kutokana na unyanyapaa ambao sasa umehusishwa na corona, itakuwa vigumu kuwashawishi wazazi ambao watoto wao wanasomea katika shule 460 kote nchini zinazotumiwa kama karantini kuwarejesha huko. Hofu kama hiyo bila shaka itawapata walimu, ikizingatiwa kuwa bado kuna uhaba mkubwa wa vifaa vya kujikinga dhidi ya maambukizi.

Huku Rais Kenyatta akikiri kuwa mpango wa serikali kuendeleza uchunguzi watu wengi unazongwa na changomoto ya uhaba wa vifaa, ina maana kuwa mkondo wa kuenea kwa virusi hivyo hautavunjwa hivi karibuni. Hii ndio maana itakuwa hatari kubwa kwa serikali kufungua shule, hata kwa watahiniwa pekee.

Pia serikali ijue sio watahiniwa wote wanaofaidi kutokana na vipindi vya masomo vinavyopeperushwa kupitia redio, runingana mitandao kama ambavyo Pro Magoha anadai.

Hivyo ni lazima kuwa na mpango mahsusi wa kuhakikisha masomo yataendelea kuanzia mahala ambapo yalisimama shule zilipofungwa.

*Wasongaco@gmail.com*

# *Vijana wakome kufanyia mzaha janga la virusi hatari*

**NA FAUSTINE NGILA**

INASIKITISHA mno kuwaona vijana wakiendelea kupuuza maagizo ya serikali yanayonuia kupunguza maambukizi ya virusi vya corona.

Baadhi ya vijana niliosema nao kwenye mitandao ya kijamii wamedai eti serikali inawalazimisha kununua maski.

Wanasema hii ni mbinu ya wafanyabishara na serikali kuwapunja wananchi na kwamba hawaina haja ya kununua maski.

Mapuuza ya kipekee hayo. Hawajui kwamba wanaambia wanunue kifaa hicho kwa manufaa yao wenyewe, kwa afya yao wenyewe.

Baadhi ya wanaofanya biashara ya teksi pia wamelalamika kuwa serikali inawazimia riziki kwa kuwataka kubeba abiria mmoja pekee badala ya wanne. Wanataka kila kiti kwa gari ndogo kiwe na mteja!



**VIJANA wakikamawa na polisi kwa kupuuza sheria za kuzuia ueneaji wa virusi vya corona.** *Picha/Maktaba*

Hivi najiuliza, upuuzi huu miongoni mwa vijana wakati vifo kutokana na virusi vya corona vimezidi 120,000 dunia, unatoka wapi?

Kuna wale wanaojishasha kuwa wao wana nguvu za kutosha mwilini na kuwa ugonjwa huo unawaua watu wazee.

Wengine wanasema virusi hivyo ni vya wale waliotangamana na watu waliosafiri mataifa ya nje.

Nawashangaa hawaelewi kati ya visa tulivyo navyo humu nchini, vingi ni maambukizi miongoni mwa watu ambao hawana historia ya kusafiri ng'ambo.

Kisha kuna wale vijana ambao wakitengwa kwa lazima wanageuza maeneo hayo kuwa ya burudani, ambapo wananunua pombe na kuandaa ngoma na densi kiholela huku wakipigana busu bila kujali.

Yaani ujinga wa kiwango hicho unawaingia vijana waliosoma, na kujihatarisha bila kukumbuka kuwa taifa la Amerika, kwa mfano, watu 1,800 hufariki kila siku.

Wengine nao wanapenda kukimbizana na polisi ili waonekane mabingwa wa mtaa, kwa kukaidi kutii kanuni za kafyu huku wenzao wakitumia njia za msituni kusafiri mashambani.

Ni kizazi ambacho hakiwezi kutulia, licha ya Waziri wa Afya Mutahi Kagwe kukiomba kisaidie kupunguza kueneza virusi hivi.

Umri wa wastani nchini Kenya ni miaka 19, lakini hiyo haimaanishi kuwa walio na umri huo hawawezi kufariki kutokana na virusi vya corona.

Inakera sana kuwa vijana mpaka sasa hawajasikia anachokariri Bw Kagwe kila anapotoa takwimu mpya kuhusu ugonjwa huo.

Labda adhabu iliyowekwa ya faini ya Sh20,000 na kifungo cha miezi sita kwa wanaopatikana katika maeneo ya umma bila maski haitoshi na yafaa kuongezwa.

Tusiwe mabaradhuli wasiosoma chochote kutokana na mataifa yalioathirika zaidi kama Amerika, Italia, Uhispania na Ufaransa.

Ole wenu vijana msiosikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini! Usimlaumu yeyote ukijipata taabani.

**MACHANGA, Embu**

# Jamaa aona moto kwa kumpa mke wa jirani pesa

KISANGA kilitokea hapa majirani wawili waliporukiana na kupigana mmoja alipogundua mwenzake alimpatia mke wake pesa akasukwa.

Minong'ono inaarifu jamaa alichemka alipompata mkewe amesukwa baada ya kuzozana na alipokataa kumpatia pesa za nywele.

"Ulitoa wapi pesa za kusukwa?" jamaa alimfokea mkewe.

Jombi alipokuwa akimgombeza mke wake, jirani yake aliingilia kati na kumtaka aache kumsumbua mwanadada.

"Ni mimi niliyempatia pesa za kusukwa baada ya wewe kumpuuza," jirani alimwambia jamaa.

Mwenye nyumba alipandwa na hasira za mkizi na wakaanza kupigana.

Ilibidi majirani kuingilia kati kuwatenganisha wanaume hao.

*Na John Musyoki*

## Wazo Bonzo




# Mama karibu achome ploti akiteketeza chupi

**KAEWA, MASINGA**

**NUSURA** mwanamke ateketeze ploti nzima akichoma chupi za mumewe zilizochakaa.

Duru zinasema kalameni na mkewe walikuwa wakizozana kila mara mama alipojaribu kumwambia mumewe anunue chupi mpya.

Tabia ya kalameni ya kuvaa chupi zilizoraruka ilimkera sana mkewe na akaamua kuzichoma.

Siku ya kisanga, kalameni alikuwa kazini mkewe alipokusanya chupi zote zilizoraruka na kuziweka katika kona ya ploti, akazimwagia mafuta taa na kuwasha moto.

Kwa sababu ya mafuta taa na upepo, moto ulisambaa na kuchoma paa ya ploti lakini majirani wakasaidiana kuuzima huku wakimfokea mwanadada kwa tukio hilo la kuhatarisha maisha na mali yao.

*Na Mirriam Mutunga*

# Aapa wazazi hawatapata mahari

**SINOKO, Bungoma**




MWANADADA aliwashangaza wengi alipoapa kuwa wazazi wake hawatapata mahari yake kwa sababu walimlazimisha aolewe.

Kulingana na mdokezi, kipusa hakufurahishwa na namna wazazi wake walivyomlazimisha kuolewa.

Inadaiwa kidosho hakuwa tayari kuolewa, lakini wazazi walimlazimisha aolewe baada yake kupotea nyumbani kwa siku tatu.

"Tunajua utokako. Rudi huko mara moja," kipusa alifokewa.

Inadaiwa kipusa alikuwa akitoka kwa mpenzi wake.

"Hakuna haja ya wewe kuendelea kuishi hapa ilhali unaenda kisiri kwa bwana yako. Nenda ukae naye," wazazi walimwambia.

Mwanadada alijaribu kujitetea lakini wazazi walikuwa wameamua.

Alipoona mambo yanazidi kuharibika, kipusa aliingia chumbani mwake na kuchukua nguo zake na kuondoka.

"Nimeenda. Sitaki kuwaona kwangu mkitafuta usaidizi wowote," kipusa alisema.

Wazee hawakutaka kusikia lolote kutoka kwake.

"Tunakusaidia upate kwako haraka badala ya kushinda ukienda kwa mwanamume huyo kila siku na kurudi hapa," walimweleza.

Inasemekana mwanadada aliendelea kurusha cheche za maneno bila kukadiria athari ya kauli zake.

"Pia ninataka msikie vizuri. Mmenilazimisha kuolewa. Mahari kutoka kwa bwanangu msahau. Hamuwezi kunifukuza kama mbwa," kipusa aliwaonya wazazi wake.

Inadaiwa baba yake alimtahadharisha dhidi ya kutoa kauli zinazoweza kumfanya ajute baadaye.

"Nimesema na nitarudia. Mimi na bwanangu hatutaleta chochote hapa. Hata paka hamtapata," mrembo aliapa huku akienda.

*Na Tobbie Wekesa*

# Polo akemewa kwa 'kukaliwa chapati'

**GELEGELE, SOTIK**

**POLO** alikemewa na ndugu zake kwa kumweleza mkewe siri za mkutano waliofanya kama wanaume wa boma.

Duru zasema mkutano huo uliitishwa baada ya hofu kutanda kuwa mmoja wao anatawaliwa na mkewe hadi akawa hana sauti katika masuala muhimu .

Mkutano uliandaliwa haraka na mbinu kadhaa za kuhakikisha kuwa kila mwanamume atakuwa simba kwake zikajadiliwa kwa kina, na kupitishwa kuwa kila mmoja azitekeleze kikamilifu.

"Siku iliyofuata, wanawake katika boma hilo walisikika wakijadili yote yaliyopitishwa na kidole cha lawama kikaelezwa kwa jamaa 'aliyekaliwa chapati' kwa kumweleza mkewe siri za wanaume wa boma lao na akaonywa vikali sana," mdokezi aliarifu.

*Na Nicholas Cheruiyot*

## Vituko vya Pokoyoyo

*Na Wycotie...*



Barua zote kwa Mhariri lazima ziwe na jina kamili la mwandishi na anwani yake. Zitumwe kwa: Mhariri, Taifa Leo, S.L.P. 49010, GPO 00100, Nairobi au tumia simu kutuma barua yako isiyopungua maneno 100 kwa nambari 20684 au barua pepe taifa@ke.nationmedia.com

# Shule zisitumiwe kuwatenga watu wanaoshukiwa kuambukizwa

AMRI iliyotolewa na serikali kuu kwa zile za kaunti kutambua shule 20 kila moja ili zitumike kama vituo vya kuwatenga wagonjwa wa virusi vya corona, inafaa kubatilishwa.

Uamuzi huo haufai ikizingatiwa kwamba Rais Uhuru Kenyatta hivi majuzi kwenye mahojiano na wanahabari aliashiria kuwa huenda watahiniwa wakaruhusiwa kurejea shuleni hivi karibuni.

Tayari taasisi 460 za elimu zimeteuliwa kutumika kuwatenga wagonjwa wa virusi hivyo maeneo mbalimbali nchini.

Badala ya kushikilia uamuzi wa kutumia shule, serikali inafaa kutafuta maeneo mengine kuwatenga watu hawa kwa sababu kila mtu anaunga mkono na anapigania ufanisi wa vita dhidi ya virusi vya corona.

Pia serikali inafaa ianze kunyunyiza dawa kwenye shule ambazo zimeanza kutumika kuwatenga wagonjwa wa virusi vya corona. Hii itahawahakikishia wanafunzi wanaorejea shuleni usalama wao wa kiafya. Hospitali za Wilaya na zahanati zinafaa zitumike kama maeneo mbadala ya kuwatenga.


*PURITY KINUTHIA, Nakuru*

## Nyoro amalize tatizo la barabara

IWAPO Gavana wa Kiambu, Dkt James Nyoro amekuwa akifuatlia habari za hapa nchini, basi anafaa kufahamu kwamba hakuna mwezi ambao hupita bila wakazi kulalamikia barabara mbovu kwenye kaunti hiyo.

Barabara hizo hupitia maeneo ambayo yanasifika kutokana na kilimo kilichonawiri, na mazao yanayosafirishwa maeneo mengine hutokea huko. Mvua inayoendelea kunyesha kwa sasa inazidisha uharibifu huo, huku raia nao wakiendelea kulalamikia hali yao inayofanya usafirishaji wa vyakula kuwa jambo gumu. Dkt Nyoro anafahamu matatizo haya kwa kuwa alihudumu kama Naibu Gavana kwenye utawala fupi wa Ferdinand Waititu aliyebanduliwa mamlakani. Dkt Nyoro ana rasilimali na ujuzi wa kutosha kuwahudumia

*DAVID KIGO, Nairobi*




## Watu wengi wapimwe corona

NJIA pekee ya kuhakikisha kwamba tunapiga hatua katika kupambana na janga la virusi vya corona ni kuwapima watu wengi mno.

Hii ni kwa sababu baadhi ya nchi ambazo zimewapima watu wengi wanaendelea kupiga hatua na kuvishinda vita dhidi ya virusi hivyo vya maangamizi.

Gonjwa hili ni vigumu kulidhibiti kwa sababu wale ambao wanaonyesha dalili ya kuwa nalo hutengwa ili wasiwaambukize wengine huku wasionyesha dalili wakilieneza kwa wengine bila kufahamu.

Serikali inafaa itafute vifaa vya kutosha kuwapima watu virusi vya corona ili tufahamu takwimu za kweli.

Wakati huo huo raia nao wanafaa kutii na kufuata maagizo ya wizara ya afya kuzuia maambukizi zaidi.

*KIMANI MEJA NJUGUNA, Kiambu*

## Kafyu hii haingerefushwa

RAIS Uhuru Kenyatta hakufaa kuongeza muda wa kafyu kwa siku 21 zaidi kwa sababu serikali yake imeshindwa kuwatimizia raia wengi mambo ya kimsingi. Wengi bado wanatatizika kupata vyakula, kazi zimeharibika na kafyu hii itaendelea kuwaongezea matatizo tele. Hakuna haja ya kuweka kafyu na kutotimizia raia maslahi yao. Badala yake, anafaa kuagiza shughuli zirejelewe kama kawaida huku raia wakitii agizo na kufuata mikakati ya kuzingatia usafi iliyotolewa na Wizara ya Afya.

*JOSEPH NDILINGE, Embu*

## Hatuwezi kuziba pengo la Ken

ITACHUKUA miaka mingi kwa taifa hili kumpata mwandishi mahiri kama marehemu Prof Ken Walibora ambaye alizikwa nyumbani kwao Cherangany wiki jana.

Vitabu vyote alivyoandika Prof Walibora vilikuwa vitabu vya haiba ambavyo vilikuwa na mafunzo tele katika jamii.

Aidha, msuko na mtiririko wa simulizi zake ulikuwa na mnato huku akiwasawiri wahusika kwa mtindo wa kipekee.

Japo ametuacha kwa kifo kichungu kutokana na ajali ya barabarani, kazi zake zitadumu milele na kunufaisha wengi.

Ninapendekeza riwaya yake ya Siku Njema iigizwe kama njia ya kumpa heshima kuu na kutambua kazi zake.

*KINYUA KING'ORI, Wakita, Voi*

## Milolongo hii itaeneza virusi

MILOLONGO ya magari inayoshuhudiwa katika miji ya mipakani ya Busia na Malaba inazua wasiwasi kwa sababu huenda ikachangia kuenea kwa corona.

Wengi wa madereva hawa hutokea katika miji ya Mombasa na Nairobi ambako maambukizi mengi ya virusi vya corona yameripotiwa kwa wingi.

Madereva wa malori hayo na mataniboi huchukua muda wa siku mbili kabla ya kuvuka mpakani na kuingia Uganda.

Wao hutangamana na wakazi wa miji hiyo miwili, na iwapo baadhi yao watapatikana na virusi hivyo, basi watu wengi wataambukizwa zaidi.

*SAMMY OBUHUMAS, Busia*

## Ujumbe Mfupi

**MAONI**: RAIS KENYATTA Jumamosi aliongeza marufuku ya kutotoka nje usiku kati ya saa 1.00 jioni na saa 11.00 alfajiri kwa siku 21 zijazo. Kadhalika, aliongeza kwa muda sawa marufuku ya kutotoka au kuingia jijini Nairobi, Mombasa, Kwale na Kilifi. Je, kafyu na marufuku ya kutoingia au kutoka katika miji hiyo imekuathiri vipi?

Ninaunga mkono hatua ya serikali kuweka kafyu kuanzia saa moja jioni hadui saa 11 alfajiri. Hii ni kwa kuwa hatua hii imesaidia sana kupunguza maambukizi ya virusi vya corona kote nchini. Vile vile, hatua ya kuzuia Wakenya kutoka ama kuingia katika kaunti za Nairobi, Mombasa, Mandera, Kilifi na Kwale ni nzuri ingawa baadhi ya maafisa wa serikali wanachukua hongo ili kuwaruhusu baadhi ya watu kukiuka agizo hilo.

***Samuel Plumber Muchiri, Karumandi.***

Nilikuwa napenda sana kutembea saa za usiku kwani iliniwezesha kufanya mazoezi kukabili maradhi ya msisimko wa damu. Hata hivyo, juhudi ambazo zimewekwa na serikali kudhibiti maambukizi ya corona zinafaa.

***Masega Daniel Manali***

Nairobi na Mombasa ndiko kitovu cha biashara humu nchini. Hivyo, marafuku ya kuingia au kutotoka ndani ya miji hii inamaanisha kuwa uchumi wa nchi nzima umeathirika.

***Peter Onesmus***


Hiyo kafyu inaharibu uchumi kote kote kwani wakati huu watu wengi hawana ajira. Maisha kwa sasa ni magumu sana.

***Abdirahman Bulare***

**MJADALA WA LEO:**
SERIKALI mnamo Jumapili ilitangaza kuongeza muda ambao wanafunzi wamo nyumbani kwa mwezi mmoja zaidi, hilo likimaanisha kwamba watakaa nyumbani hadi Juni. Waziri wa Elimu Prof George Magoha alisema kuwa hatua hiyo inalenga kuwalinda wanafunzi dhidi ya maambukizi ya virusi vya corona. Je, kwa maoni yako, unaunga mkono hatua hiyo?

**KUWASILIANA**
**Tutumie maoni yako kuhusu mjadala huu kwa nambari ya simu 20684 au barua pepe taifa@ke.nationmedia.com na tutachapisha kesho baadhi ya maoni tutakayopokea.**

## FUMBO



**KULIA:**
1. Tamko linalotumiwa na mganga ili kuwafanya watu wamsikize.
4. Watoto waliozaliwa kutokana na mimba moja.
7. Uelekeo fulani.
8. Kukosa kutosha kwa nguo kwa sababu ni kubwa.
9. Muda wa dakika sitini.
12. Mkusanyiko wa watu walioungana kwa lengo fulani.
13. Kinyume cha "hafai".
15. Kanusho la kusema "niuhai".
16. Isiyo rahisi.
17. Umio
20. Bidii au jitihada.
21. Mahaba
22. Ala ya muziki kama kinanda.
23. Mtu mwenye madaraka katika ofisi.

**CHINI:**
1. Isiyo na kitu ndani.
2. Kinyume cha "usiione".
3. Weka karibu na barabara au paki.
4. Meno yaliyopandana.
5. Mojawapo ya ngoma maarufu zinazochezwa na wanawake wa Pwani ya Afrika Mashariki.
6. Kinyume cha "anapakua".
10. Enda huku na huko kwa sababu ya shughuli.
11. Ona wasiwasi.
14. Atega sikio ili apate kuyapata tunayozungumza.
15. Harufu ya samaki baada ya kuvuliwa.
18. Kinywaji kinachotokana majani ya mchai.
19. Mnyama wa mfugo anayesaidia watu kuwinda na kulinda

### FUMBO LA JANA

| KULIA: | CHINI: |
|---|---|
| 1. Legea | 1. Lala |
| 4. Zaidi | 2. Gana |
| 7. Mlango | 3. Aporwa |
| 8. Mchai | 4. Zamisha |
| 9. Rai | 5. Idhiniwa |
| 12. Sinia | 6. Alikataa |
| 13. Elekea | 10. Jemadari |
| 15. Namwia | 11. Jenereta |
| 16. Apewa | 14. Egamika |
| 17. Mui | 15. Nyimbo |
| 20. Ajemi | 18. Kama |
| 21. Mwanga | 19. Ngaa |
| 22. Ibada | |
| 23. Onana | |

## Vitendawili na Methali

### METHALI

1.................... huishia ngokoni
2. ..................hawakai zizi moja
3. Fedha................
4. Figa moja, ...............
5. Fimbo ya mbali .........
6. Fimbo la mnyonge.........

### VITENDAWILI

1. Huna macho lakini wakamata wanyama.
2. Hupanda mtini na mwenye kichaa wake.
3. Hutembea watatu.
4. Hutoka upesi sana lakini hasalimu.
5. Huwafanya watu wote walie.
6. Huwezi kukalia alipokalia msichana wangu mweusi.

**MAJIBU YA METHALI**
1. Faragha ya nyani
2. Fahari wawili
3. fedheha
4. haliinjiki chungu.
5. haiuwi nyoka
6. mifi Mungu.

**MAJIBU YA VITENDAWILI**
1. Ndoana
2. Kivuli
3. Mafiga
4. Kuku
5. Moshi
6. Chungu jikoni

# Afya Jamii

Toleo 039



# Corona pigo kwa afya ya uzazi

*"Afya ya uzazi ni mojawapo ya huduma ambazo zitaathirika pakubwa kutokana na mkurupuko wa maradhi ya Covid-19"*

*Dkt Natalia Kanem (Mkurugenzi Mtendaji, UNFPA )*

UK12-13

## Yaliyomo

Sintofahamu kuhusu tiba ya Covid-19
UK14

Unywaji pombe ukiwa na HIV hudhoofisha mifupa
UK14

Nation Media Group "Digital Copy"

# Mkurupuko wa Corona pigo kwa wajawazito

*Japo kuna data chache kuhusiana na athari za maradhi ya COVID-19 kwa wanawake wajawazito, wataalamu wanahofia huenda marufuku ya kutotoka nje ikasababisha ongezeko la vifo vyao pamoja na watoto*



NA PAULINE ONGAJI

Wiki tatu hazijakamilika tangu Mati Nyamai, 45, kumzika marehemu mkewe, Lydia Nduku Mati, 41, lakini bado hajapata muda wa kuombeleza.

Bw Nyamai, ambaye ni mkandarasi kutoka kijiji cha Kiimani, kaunti ndogo ya Mbuinzau, Kaunti ya Makueni, anakabiliwa na kibarua kigumu cha kuwalea wanawe sita, vile vile kuwasaidia kukubali uhalisia wa kifo cha ghafla cha mama yao.

Marehemu Lydia alifariki Machi 31 baada ya kuvuja damu alipokuwa akijifungua mtoto wao wa saba, ambaye pia alifariki.

"Mke wangu alitarajiwa kujifungua mnamo Machi 31 kulingana na ratiba ya kliniki. Hata hivyo mnamo Machi 30 mwendo wa saa tano usiku alianza kukumbwa na maumivu tuliyoamini kuwa uchungu wa uzazi. Lakini kutokana na sababu kuwa tayari yalikuwa masaa ya marufuku ya kutotoka nje, hatungeweza kwenda hospitalini. Pia, hakukuwa na mbinu ya usafiri kuelekea katika kituo cha matibabu, kilicho umbali wa kilomita tatu kutoka nyumbani," anaeleza.

Ili kukabiliana na maumivu, anasema, marehemu mkewe alimshauri ampeleke kwa mkunga maarufu kijijini ili atumie utaalamu wake kupunguza uchungu, huku akisubiri kwenda hospitalini keshoye.

"Tulilazimika kukatiza vichakani na giza hadi nyumbani kwake ambapo mkunga huyo alifaulu kumpunguzia maumivu. Mambo yalirejelea hali ya kawaida lakini mwendo wa saa tisa alfajiri Machi 31 tukiwa nyumbani, alianza kuvuja damu kutoka ukeni," anakumbuka.

Kulingana na Bw Nyamai, haya yaliendelea hadi mwendo wa saa kumi na moja asubuhi (mwisho wa masaa ya kafyu) ambapo walifaulu kumpata mwendesha bodaboda aliyempeleka marehemu Lydia katika hospitali ya kaunti ndogo ya Kibwezi.

"Aliwekwa kitandani kwa saa moja ambapo baadaye walimpeleka katika thieta. Baada ya muda, daktari alirejea na kutuambia kwamba mtoto alizaliwa akiwa amefariki baada ya kusakamwa na damu akiwa tumboni," aeleza.

Kwa upande mwingine, daktari alisema kwamba marehemu Lydia alikuwa katika hali mbaya kwani alikuwa amepoteza kiwango kikubwa cha damu, na hivyo alihitaji kuongezewa.

"Lakini tena akasema kwamba hospitali hiyo haikuwa na damu na hivyo ilibidi watafute. Mwendo wa saa nane adhuhuri walituarifu kwamba tayari walikuwa wamepata damu kutoka eneo la Voi na kwamba ambulansi ilikuwa njiani kwenda kuleta bidhaa hiyo," aeleza.

Hata hivyo, mwendo wa saa kumi jioni; hata kabla ya ambulansi kufika hospitalini, Bw Nyamai anasema walipokea taarifa za huzuni kutoka kwa daktari kwamba mkewe alikuwa ameaga dunia.

"Daktari alituandikia idhini ya kuturuhusu kurejesha mwili wake nyumbani na siku iliyofuatia - chini ya masaa 24 baada ya kifo chake, tukamzika, pasipo ibada yoyote ya wafu wala upigwaji picha, kuambatana na utamaduni wetu," aongeza.

Anasema kwamba bado hajaamini kwamba mkewe hayupo tena, lakini anasisitiza kwamba hana muda wa kuwazia hayo hasa wakati huu wa janga la maradhi ya Covid-19.

Kwa sasa anasema mawazo yake yote ameyaelekezea wanawe kwani ndiye mama na baba. "Japo sijarejea kazini, nitakapohitajika kufanya hivyo, nitalazimika kukaa masaa mengi kazini na bado najiuliza maswali kuhusu jinsi nitakavyoweza kufanya hivyo na kuwatunza wanangu pia," aeleza.

Bw Nyamai anaamini kwamba mambo yangekuwa tofauti endapo mkewe angefikishwa hospitalini pindi alipoanza kukumbwa na uchungu wa uzazi licha ya marufuku ya kutotoka nje, au endapo angepokea damu pindi alipofika hospitalini. "Naamini kwamba hangefariki," asisitiza.

Japo kuna data chache kuhusiana na athari za maradhi ya COVID-19 kwa wanawake wajawazito, wataalamu wanahofia kwamba hatua ya marufuku ya kutotoka nje, iliyochukuliwa na mataifa mbalimbali ili kupunguza usambazaji wa maradhi haya, yaweza sababisha ongezeko la vifo vya wajawazito na watoto wakati wa kujifungua.

Wanatabiri haya kuambatana na matukio ya yaliyoshuhudiwa wakati wa mkurupuko wa maradhi ya Ebola katika baadhi ya mataifa ya Afrika Magharibi kati ya mwaka wa 2014 na 2016.

Mwaka wa 2015, UNFPA ilitabiri kwamba mkurupuko huo ungesababisha vifo 120,000 vya wanawake wajawazito na watoto wakati wa kujifungua.

Juma lililopita, Dkt Natalia Kanem, Mkurugenzi Mtendaji wa UNFPA, alitaja afya ya uzazi kuwa mojawapo ya huduma ambazo zitaathirika pakubwa kutokana na Covid-19.

Dkt Jemimah Kariuki, mtaalamu wa masuala ya uzazi na mwanajinalokojia anasema kwamba itakuwa vigumu kuzuia ongezeko la idadi ya vifo vya wanawake na watoto wakati wa uzazi, ikiwa hakuna atakayeingilia kati na kuhakikisha kwamba wanawake wajawazito wanapokea huduma wanazohitaji.

"Kuna uwezekano mkubwa kwamba wanawake wajawazito hawataenda hospitalini au kufika wakiwa wamechelewa wakihofia kuambukizwa maradhi haya katika vituo vya kiafya. Hii inamaanisha kwamba kutakuwa na ongezeko la idadi ya akina mama watakaojifungua wakiwa nyumbani, suala litakalowaweka katika hatari zaidi," aongeza.

Sio hayo tu, Dkt Kariuki anasema kwamba mara nyingi wakati wa mkurupuko, rasilimali nyingi huondolewa kutoka huduma za uzazi na kuelekezewa sehemu zingine zinazodhaniwa kuwa za dharura.

"Tayari hospitali ya Kaunti ya Mbagathi imetengewa matibabu dhidi ya maradhi haya. Hali hii ni sawa katika baadhi ya sehemu za hospitali ya Kitaifa ya Kenyatta. Naelewa umuhimu wa hatua ya serikali, lakini hospitali hizi hushughulikia idadi kubwa ya wanawake wajawazito, suala ambalo bila shaka litaathiri kutolewa kwa huduma hizi," aeleza.

Kwa sasa Dkt Kariuki asema zahanati, kliniki na vituo vingine vya kiafya vinapaswa kushughulikia visa vya kawaida vya kujifungua, huku wajawazito wanaohitaji huduma za dharura pekee wakiruhusiwa kwenda katika hospitali za viwango vya juu. Hii itazuia msongamano katika hospitali hizi hasa wakati huu wa janga la corona," aeleza.

Dkt Kariuki ambaye mnamo Aprili 7, 2020 alianzisha kampeni za kusaidia wanawake wajawazito kufikia huduma za uzazi wakati huu anachelea kwamba kuna uwezekano wa akina mama kumiminika hospitalini licha ya kutokumbwa na dharura.


"Nimesikia visa kuhusu wanawake waliojawa na hofu wanaoenda hospitalini usiku licha ya kutokumbwa na uchungu wa uzazi wala hali ya dharura yoyote. Wengi wanakwamilia hospitalini baada ya kuambiwa warejee nyumbani," aongeza.

Kulingana na Dkt Kariuki, ili kujiepusha na hali ya aina hii, wanawake wajawazito wanaweza tumia huduma za kuwasiliana kwa majukwaa ya kieletroniki (telemedicine), kuzungumza na madaktari wao kuhusu masuala madogo madogo ya kiafya, na hivyo kuzuia mtagusano usiohitajika.

Pia, anasisitiza haja ya kuwaelimisha kuhusu wanachopaswa kufanya wanapohisi namna fulani, vile vile dalili za kukumbwa na hali ya dharura ili waweze kufika hospitalini kwa wakati

**120,000**

Utabiri wa UNFPA 2015 kuhusu idadi ya vifo vya wanawake wajawazito na watoto wakati wa kujifungua wakati wa mkurupuko wa Ebola katika baadhi ya mataifa ya Afrika Magharibi



**"Kuna uwezekano mkubwa kwamba wanawake wajawazito hawataenda hospitalini au kufika wakiwa wamechelewa wakihofia kuambukizwa maradhi haya katika vituo vya kiafya. Hii inamaanisha kwamba kutakuwa na ongezeko la idadi ya akina mama watakaojifungua manyumbani, suala litakalowaweka katika hatari zaidi.**


**-Dkt Jemimah Kariuki**
*(Mwanajinakolojia)*

**Mhariri Mkuu:** Mutuma Mathiu **Mhariri:** Peter Ngare **Mhariri wa Makala:** Muthoni Kariuki **Mhariri Msaidizi:** Fatuma Bariki **Mhariri wa Picha:** Joan Pereruan **Msanifu Kurasa Mkuu**: Andrew Anini **Wasanifu Kurasa:** Alice Othieno, Joy Abisagi, Eliud Maumo, Lisa Wamugunda, Allan Omondi na Benjamin Situma **Waandishi:** Pauline Ongaji, Benson Matheka, Bernadine Mutanu, Leonard Onyango na Mary Wangari.

ufaao kabla ya masaa ya kafyu.

Ili kuzuia balaa kama iliyoshuhudiwa katika mataifa ya Magharibi mwa Afrika wakati wa mkurupuko wa Ebola, Dkt Kariuki anapendekeza kuajiriwa sio tu kwa madaktari zaidi, bali pia wahudumu wengine wa kiafya.

"Utambuzi mmoja wa virusi vya corona hospitalini unalazimu wahudumu wa kiafya waliomshughulikia mhusika kuwekwa kwenye karantini ya lazima, suala linaloathiri hata zaidi idadi ya wahudumu wa kiafya. Kutokana na sababu hii, madaktari na wahudumu zaidi wa kiafya wanapaswa kuajiriwa hata katika viwango vya kaunti, pindi wanapokamilisha masomo," aongeza.



## Afya ya Uzazi

# Idadi ya vifo vya wajawazito ingali juu katika mataifa yanayostawi

### Takwimu

**38%** — Idadi ya vifo ilipungua ulimwenguni kati ya 2000-2017

**94%** — Idadi ya vifo kutokana na mapato ya nchi

**86%** — idadi ya vifo katika Mataifa yaliyoko kusini mwa jangwa la Sahara na Kusini mwa bara Asia

**75%**

*Matatizo mengi ambayo huwakilisha takriban asilimia 75 ya vifo vyote vya aina hii ni:*

- Kuvuja damu nyingi (hasa wakati wa kujifungua)
- Maambukizi (hasa baada ya kujifungua)
- Shinikizo la damu wakati wa ujauzito (pre-eclampsia na eclampsia)
- Matatizo wakati wa kujifungua
- Kuavya mimba kwa njia isiyo salama
- Matatizo yaliyosalia husababishwa au huhusishwa na maambukizi kama vile maradhi ya malaria, au maradhi ya moyo na kisukari.

**Chanzo:** Shirika la Afya Duniani

KULINGANA na Shirika la Afya Duniani, kati ya mwaka wa 2000 na 2017, idadi ya vifo vilivyotokea miongoni mwa wanawake wajawazito na watoto wakati wa kujifungua vilipungua kwa 38% ulimwenguni kote.

Lakini licha ya haya, taarifa hizi zinaonyesha kwamba idadi ya visa hivi bado iko juu. Kulingana na WHO, mwaka wa 2017 ilikadiriwa kwamba kila siku takriban wanawake 810 ulimwenguni kote walifariki kutokana na matatizo wakati wa ujauzito na kujifungua.

Hii ni sawa na takriban wanawake 295 000 mwaka huo. Aidha, kulingana na ripoti hiyo, idadi kubwa ya vifo hivi (94%) vilitokea kutokana na mapato ya chini, huku takwimu zikionyesha kwamba asilimia kubwa ya visa hivyo vingezuiwa.

Kadhalika idadi kubwa ya vifo hutokea katika mataifa yenye mapato wastani na ya chini. Aidha, vijana katika umri wa kubalehe (kati ya miaka 10 na 14) wamo katika hatari kubwa ya kukumbwa na matatizo na hata vifo wakati huu, wakilinganishwa na wanawake wengine.

Mataifa yaliyoko kusini mwa jangwa la Sahara na Kusini mwa bara Asia yaliwakilisha 86% (254 000) ya idadi ya vifo hivi mwaka wa 2017. Mataifa ya Kusini mwa jangwa la Sahara pekee yaliwakilisha takriban theluthi mbili ya visa hivi (196 000), huku nchi za Kusini mwa Asia zikiwakilisha humusi ya idadi hiyo (58 000).

Kwa mujibu wa takwimu hizi, idadi kubwa ya vifo hutokea katika baadhi ya maeneo duniani yanayoakisi kutokuwepo kwa usawa katika huduma za afya, na hivyo vinaangazia mwanya uliopo kati ya maskini na matajiri.

Idadi ya vifo hivi katika mataifa ya mapato ya chini, mwaka wa 2017 ilikuwa 462 kwa watoto 100,000 waliozaliwa wakiwa hai, ikilinganishwa na visa 11 kwa watoto 100 000 wanaozaliwa wakiwa hai katika mataifa ya mapato ya juu.

**Kwa hivyo kwa nini wanafariki?**

Wanawake hufa kutokana na matatizo wakati wa ujauzito na kujifungua. Matatizo mengi hutokea wakati wa ujauzito na mengi yanaweza zuiwa na kutibiwa. Kuna baadhi ya matatizo ambayo hukuwepo hata kabla ya ujauzito, lakini huzidi kuwa mabaya ikiwa hayatadhibitiwa.

**Je, kwa nini hawashughulikiwi kama inavyohitajika?**

Wanawake maskini hasa katika maeneo ya mbali wamo katika hatari kubwa ya kutopokea huduma za afya wakati wa ujauzito. Hali hii ni halisi hasa katika nchi ambapo kuna upungufu wa wahudumu wa kiafya, hasa mataifa ya Afrika yaliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara na Kusini mwa Asia.

Data zilizopo zinaonyesha kwamba katika mataifa mengi ya mapato ya juu au wastani, zaidi ya 90% ya wanawake wanaojifungua hunufaika kupata huduma za mkunga aliyepokea mafunzo, daktari na mhudumu wa afya.

Hata hivyo, chini ya nusu ya akina mama wanaojifungua katika mataifa kadhaa ya mapato ya chini, ndio wanaobahatika kupokea huduma za wataalamu hawa.

**Masuala hususan yanayozuia wanawake kupokea huduma wakati wa ujauzito na kujifungua ni:**

1. Umaskini
2. Mwendo mrefu kufikia vituo vya afya
3. Kutojua
4. Kiwango duni au ukosefu wa huduma bora za afya
5. Imani za kitamaduni

*Na Pauline Ongaji*

Nation Media Group "Digital Copy"

# Pata ushauri wa Dkt Flo

Afya Jamii

## Kwa kifupi




### Wanasayansi watofautiana kuhusu ikiwa dawa ya Ebola yatibu Corona

WANASAYANSI wametoa ripoti zinazokinzana kuhusu ikiwa dawa ya Ebola, ***Remdesivir***, inatibu virusi vya corona au la.

Ripoti ya mwanzo ya majaribio yaliyofanywa nchini China na kuchapishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) inaonyesha kuwa dawa hiyo haitibu virusi vya corona.

Kampuni ya Gilead Sciences ya nchini Amerika iliyoitengeneza hata hivyo imepuuzilia mbali ripoti hiyo huku ikisema kwamba wanasayansi wa China waliharakisha kutoa ripoti kabla ya kumaliza kufanya majaribio.

Watafiti wa nchini China walisema kuwa dawa hiyo ilishindwa kuwasaidia wagonjwa mahututi wa virusi vya corona.

***Remdesivir*** ilitengenezwa kupambana na maradhi ya Ebola na pia ilitumiwa kutibu waathiriwa wa homa ya ***Severe Acute Respiratory Syndrome*** (SARS) ambayo virusi vyake vina sifa sawa na vile vinavyosababisha corona.

Baadhi ya madaktari wanadai kuwa dawa hiyo inasaidia kwa kiwango kikubwa iwapo wagonjwa wa corona watapewa mapema kabla ya kulemewa na virusi.

Majaribio yaliyofanywa na Chuo Kikuu cha Chicago, Amerika, yalionyesha kuwa ***Remdesivir*** iliharakisha kupona kwa waathiriwa wa virusi vya corona.

*Na Leonard Onyango*

### Unywaji pombe ukiwa na HIV hudhoofisha mifupa-Utafiti

WAATHIRIWA wa virusi vya HIV wanafaa kujiepusha na pombe ili kulinda afya ya mifupa yao, utafiti umebaini.


Utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Boston umebaini kuwa pombe huharibu protini ambayo huusika na utengenezaji wa mifupa.

Kulingana na watafiti hao, kiasi chochote cha pombe hufanya mifupa ya waathiriwa wa HIV kuwa dhaifu.

Watafiti hao walihusisha watu 198 wanaoishi na virusi vya HIV. Walibaini kuwa waathiriwa wa HIV wanaokunywa pombe walikuwa na mifupa dhaifu ikilinganishwa na wenzao wasiotumia vileo.

"Tulibaini kuwa hata wale wanaoonja kiasi kidogo cha pombe walikuwa na tatizo la mifupa dhaifu," wakasema watafiti hao.

Utafiti huo uliochapishwa katika jarida la ***Alcoholism: Clinical and Experimental Research,*** unasema kuwa idadi kubwa ya waathiriwa wa HIV wanaolewa wana mifupa dhaifu na huwa na matatizo ya kutembea kadri umri unavyozidi kuongezeka.



Watafiti hao wanasema kuwa mbali na kuwahimiza waathiriwa wa HIV kufanya mazoezi na kula vyakula vyenye vitamini D ili kuimarisha mifupa yao, wanafaa pia kuepuka kunywa pombe.

*Na Leonard Onyango*

# Miaka 19 na sijaota ndevu, tatizo nini?

***Mpendwa Daktari,***
***Je, nitakabiliana vipi na vidonda vya mafua vinavyonitoka puani kila wakati?***
***Jared, Nairobi***



**Mpendwa Jared,**
Vidonda vya mafua husababishwa na virusi vya ***Herpes Simplex***. Watu wengi huambukizwa maradhi haya wakiwa utotoni na watoto wenzao, ambapo virusi hivi hujificha mwilini na kujitokeza unapokumbwa na msongo wa mawazo, ukiwa na mafua au mabadiliko ya kihomoni mwilini. Haiwezekani kukabiliana kikamilifu na vidonda hivi, lakini waweza kuvidhibiti kwa kutumia krimu za kupunguza uvimbe au dawa za kupunguza makali ya virusi hivi kwa ushauri wa daktari. Ukiwa na vidonda vya mdomoni, fukuta mchanganyiko wa maji yaliyopashwa moto na chumvi au dawa maalum ya mdomoni, jiepushe na vyakula au vinywaji moto; usile vyakula vilivyo na chumvi, viwango vya juu vya asidi au viungo vingi. Kunywa maji mengi na udumishe afya ya mdomoni.
Aidha, waweza nufaika kutokana na vijalizo vya virutubisho vya vitamini B na *folic acid*. Ikiwa vidonda hivi vitaendelea kwa zaidi ya wiki mbili pasipo kupona, basi unahitaji kufanyiwa uchunguzi na daktari.



***Mpendwa Daktari,***
***Mimi ni kijana wa miaka 19. Nilikamilisha shule ya upili mwaka jana lakini bado sijashuhudia ndevu hata moja usoni mwangu. Ni jambo la kuaibisha hasa ikizingatiwa kwamba wenzangu wamekuwa wakinyoa ndevu kwa miaka sasa. Je, nina tatizo na ikiwa ni hivyo, nifanyeje kurejea hali ya kawaida?***
***Msomaji***

**Mpendwa msomaji,**
Ndevu ni mojawapo ya sifa za utambuzi kwa mwanamume. Sifa hii huanza kujitokeza katika umri wa kubalehe. Kuna baadhi ya wanaume ambao watajawa na ndevu wanapotimu umri wa miaka 18, ilhali kuna wengine ambao huenda wakasubiri hadi miaka ishirini au baadaye na hii ni kawaida. Kiamuzi kikubwa kinachobaini kasi cha ndevu kuota ni jeni. Hebu chunguza kutoka kwa jamaa zako wa karibu wa kiume kuhusu wakati walioota ndevu kwa mara ya kwanza. Katika umri wa miaka 40 mtu anaweza kuwa na ndevu zilizojaa ilhali zilianza kuota akiwa na miaka 34. Pili, ikiwa viwango vyako vya homoni za ***testosterone*** viko chini, basi huenda ndevu zako zikachelewa kuota au kasi ya kuota kwake ikawa chini. Hata hivyo ikiwa una viwango vya kawaida, basi vijalizo vya homoni hizi haviwezi kukusaidia.
Unaweza kaguliwa na mtaalamu wa ngozi kwa masuala kama vile matayarisho ya ngozi ambayo huenda yakachochea nywele hizi kuota. Kwa mfano kutumia krimu ya *minoxidil, 3% peppermint oil* au *micro-needling*. Pia, dumisha lishe bora, pata usingizi wa kutosha, subira na kufanya mazoezi.

***Mpendwa Daktari,***
***Nina mimba ya miezi miwili na nimekuwa nikishuhudia madoa ya damu kwenye suruali zangu kwa siku tatu sasa. Je, hii ni kawaida, na ikiwa sivyo, nifanyeje kukabiliana na tatizo hili?***
***Karen, Mombasa***

**Mpendwa Karen,**
Ni kawaida kushuhudia doa la damu wakati ambapo mimba inajitunga kwenye ukuta wa uterasi. Damu hii hutoka katika wiki za awali za ujauzito na mara nyingi huwa kidogo na huisha kivyake bila matibabu. Aidha, huenda ukavuja damu kutokana na mwasho kwenye lango la uzazi, maambukizi, mimba kujitunga nje ya uterasi (ectopic pregnancy) au hatari ya mimba kutoka. Litakuwa jambo la busara na la dharura kwako kumuona mwanajinakolojia ili ufanyiwe uchunguzi wa kimatibabu, ufanyiwe uchunguzi wa maabara na hata kupigwa picha za sehemu ya nyonga. Ikiwa mimba imejitunga nje ya uterasi na unavuja damu, upasuaji wa dharura hufanywa. Ikiwa kuna hatari ya mimba kutoka, huenda ukatibiwa na kurejea nyumbani, au ukalazwa hospitalini. Kuna wakati ambapo damu huanza kuvuja kuashiria kwamba tayari mimba imeanza kutoka, ambapo utapelekwa hospitalini na kutibiwa kwa kukamilisha shughuli hii.

***Je, una swali au jambo lolote la kibinafsi ambalo ungependa ushauri wa Daktari? Waweza kututuma ujumbe kwa barua pepe afyajamii@ke.nationmedia.com***

# Kocha aahidi kutwalia Trans Nzoia Falcons taji

Na TITUS MAERO

MKUFUNZI mpya wa Trans Nzoia Falcons FC, Christopher Amwayi ameanika azma yake akisema timu hiyo itapigania kufa-kupona ubingwa wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake msimu huu.

Amwayi aliyekuwa kocha msaidizi wa timu ya wanaume ya Transfoc FC mjini Kitale, alisema Falcons ina wachezaji wengi walio na uzoefu mwingi katika fani hiyo ya spoti. Kocha huyo alisaini kandarasi ya mwaka mmoja na Falcons inayofadhiliwa na serikali ya kaunti ya Trans Nzoia.

Amwayi alichukua usukani wa timu hiyo kutoka kwa Evans Ingosi aliyejiuzulu.

"Ninafahamu vizuri sana timu hii ya Trans Nzoia Falcons kwani nikiwa Transfoc FC tulikuwa tunafanya mazoezi ya zamu kwenye uwanja wa Kenyatta kabla ya vipusa hao kuhamia uwanja wa Kitale Manor House," alidokeza.

Katika mahojiano na *Taifa Leo* mjini Kitale jana, Amwayi alisema miongoni mwa wachezaji walio na uzoefu wa kimataifa katika timu yake ni kiungo Martha Amunyolete.

Amunyolete alijumuishwa katika timu ya taifa ya Harambee Starlets ya Kombe la Afrika (AWCON) lililoandaliwa nchini Ghana mwaka wa 2018. Nyota wengine katika kikosi cha Amwayi ni kipa Phyllis Chemtai, beki Cynthia Livondo, kiungo Linda Nasimiyu na mshambuliaji matata Tumaini Waliaula. Falcons ilimaliza msimu uliopita katika nafasi ya tatu nyuma ya Vihiga Queens ya Alex Alumira iliyohifadhi taji, na nambari mbili Gaspo Women FC.



**SHARON Mukhwana wa Trans Nzoia Falcons (kulia) apigania mpira na wachezaji wa Mathare United wakati wa mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake mwaka jana jijini Nairobi.** *Picha/ Chris Omollo*

# Klabu yaombea silaha tatu za Bandari zibakie

Na ABDULRAHMAN SHERIFF

KOCHA Mkuu wa Coast Stima FC, Paul Ongai anatamani kusalia na wachezaji watatu walioko katika timu yake kwa mkopo kutoka Bandari FC ili waisaidie kushinda taji la Ligi ya Supa inayodhaminiwa na Betika (BNSL).

Ongai aliambia *Taifa Leo* kuwa yeye anaamini wanasoka hao wataweza kuisaidia timu hiyo katika kampeni za kufuzu kushiriki Ligi Kuu msimu ujao.

Wanasoka hao ni beki Hassan Iddi, kiungo Dennis Magige na winga Joshua Oyoo.

"Ninachoomba ni Iddi, Magige na Oyoo tuwe nao na ikiwezekana tuwasajili kikamilifu kwani watatusaidia kupanda ngazi hadi," alisema mkufunzi huyo, ambaye ana uhakika watafanya vizuri ligi hiyo itakaporejelewa baada ya janga la corona.

Alisema kusitishwa kwa mechi za ligi mbalimbali kutokana na amri ya serikali baada ya mkurupuko wa ugonjwa wa virusi vya corona, kumeathiri pakubwa hali za wachezaji kwani kufanya mazoezi ya kibinafsi ni tofauti sana na kuwa na mazoezi ya pamoja.

Hata hivyo, ana matumaini wanasoka wake wanafuata mipango aliyowapangia wakati huu wachezaji wameshauriwa kubaki majumbani.

Wakati mechi zilipoyosimamishwa, Coast Stima ilikuwa katika nafasi ya nne kwa pointi 49. Nairobi City Stars inaongoza kwa alama 64 ikifuatiwa na Bidco United (54) na Vihiga United (52).

## Nyota huyo wa KCB asema alikuwa na uwezo wa kumpiku Otieno mechi zote zingechezwa

# Agwanda ataka 'umakinifu' katika kutuza mfumaji bora

Na CECIL ODONGO

MSHAMBULIAJI wa klabu ya KCB, Enock 'Jowi' Agwanda ametaka usimamizi wa Ligi Kuu ya Kenya (KPL) kutoa ufafanuzi jinsi ambavyo mshindi wa 'kiatu cha dhahabu' atakavyoamuliwa iwapo msimu huu utafutiliwa mbali kutokana na janga la corona.

Agwanda anashikilia nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora wa msimu huu kwa mabao 12. Yuko katika nafasi ya tatu nyuma ya mshambuliaji Timothy Otieno wa Tusker FC, ambaye amecheka na nyavu mara 14, na mvamizi John Makwata aliyefungia AFC Leopards mabao 13 kabla ya kuelekea nchini Zambia kujiunga na Zesco United. Enosh Ochieng' (Ulinzi Stars), Elvis Rupia (AFC Leopards) na Benson Ochieng' (Western Stima) wametikisa nyavu mara tisa kila mmoja.

Katika mahojiano, mvamizi wa zamani wa SoNy Sugar FC, Agwanda alisema hatakubali Otieno apokezwe kiatu cha dhahabu ilhali hata yeye ana uwezo wa kufunga mabao zaidi iwapo mechi 10 zilizosalia zitasakatwa zote.

"KPL ndiyo mwaamuzi kuhusu masuala haya na iwapo mechi za msimu hazitarejelewa, wanafaa kutueleza jinsi ambavyo mshindi wa kiatu cha dhahabu atakavyoamuliwa.

"Nasikia kwamba kuna sheria ambayo inatoa mwanga jinsi mshindi wa taji la Ligi Kuu anafaa aamuliwe. Je, kuna sheria za kuamua mshindi wa kiatu cha dhahabu iwapo msimu hautamalizika?" aliuliza Agwanda, ambaye pia aliwahi kuchezea Gor Mahia, ambayo haijatoa mfungaji bora tangu Mganda Dan Sserunkuma aifungie mabao 16 mwaka 2014.

Mwanadimba huyo alisema kwamba amekuwa akibadilishana uongozi na Timothy Otieno wa kutia nyavuni mabao mengi jinsi mechi zilivyokuwa zikisakatwa na itakuwa vyema iwapo mechi zote zitakamilishwa

"Sina uhasama wowote wa kibinafsi dhidi ya Timothy Otieno, lakini KPL wanafaa wafahamu kwamba kuna kipindi nilikuwa na mabao 10 yeye akiwa na manane. Je, ligi ingeishia wakati huo ningekabidhiwa tuzo hiyo?" aliuliza.

Afisa Mkuu Mtendaji wa KPL Jack Oguda hakupokea simu tulipomfikia ili atoa kauli yake kuhusu suala hilo.

Mechi za KPL zilisitishwa mwezi uliopita baada ya serikali kupiga marufuku mikusanyiko ya watu maeneo ya umma kutokana na janga la corona.



**ENOCK Agwanda wa KCB [kushoto] akifunga bao dhidi ya Western Stima katika mechi iliyopita ya KPL. Anapigania 'Kiatu cha Dhahabu' na Timothy Otieno wa Tusker FC.** *Picha/Sila Kiplagat*

# Obunga aahidi kuvumisha Zetech ligi kuu ya mpira wa vikapu

Na JOHN KIMWERE

SAJILI mpya wa timu ya wanawake ya mpira wa kikapu ya Chuo Kikuu cha Zetech, Debra Obunga amesema analenga kusaidia kikosi hicho kutwaa taji la Ligi Kuu.

Pia, amedokeza kuwa anaamini ameiva kuipiga jeki timu ya taifa aliyowahi kuichezea miaka tisa iliyopita.

"Sijawahi kupoteza imani ya kuibuka staa tangia utotoni mwangu katika mchezo wangu maana wakubwa wangu wamekuwa wakinihimiza nitie bidii michezoni," alisema na kuongeza kuwa ananuia kutumia uzoefu wake wa miaka 12 kuhakikisha Zetech inatwaa ubingwa wa Ligi Kuu.

Alidokeza kuwa hakuna kinachoweza kuzima hisia zake kuhakikisha ameshinda taji la pili raundi hii akichezea Zetech.

Mchezaji huyu anajivunia kusaidia timu ya Halmashauri ya Bandari ya Kenya (KPA) mwaka 2013 kushinda Ligi Kuu.

Nyota huyo wa zamani wa Kenya Ports Authority anaendelea na mazoezi ya kibinafsi nyumbani wakati huu ambapo janga la virusi vya corona limepangua michezo yote sehemu nyingi duniani.

Licha ya yote, Obunga anasema anaendelea kujiweka makali akisubiri michezo kurejelewa baada ya maambuziki ya ugonjwa huo kukomeshwa.

## Kwa Ufupi

MACHAKOS

### Kituli yatoka nyuma na kuwika

**TIMU** ya soka ya Shule ya Upili ya Kituli iliichabanga Kalingile FC mabao 2-1 kwenye mechi ya kirafiki uwanjani Kathese, Jumapili. Mechi ilianza kwa kishindo kikuu, huku kila timu ikijibidiisha kupata bao la mapema. Kalingile ilitangulia kuona lango dakika ya 23 kupitia kombora la mvamizi Kimeu Mutiso. Vijana wa Kituli walicheza kwa bidii ya mchwa na kupata mabao mawili ya haraka kupitia jitihada za Benard Muema na Muasya Simon katika kipindi cha lala-salama.

*Na Cornelius Mutisya*

KWALE

### Supa Matuga yategea mechi 2

**MKUFUNZI** wa Supa Matuga FC Matano Mbete amejawa na matumaini vijana wake watashinda mechi mbili za mkondo wa kwanza zilizosalia ligi ya taifa daraja la pili itakapoendelea baada ya kuisha kwa janga la corona. Mbete alisema ushindi utawezesha kupanda juu ya jedwali la ligi hiyo. "Tumesalia na mechi dhidi ya Bahari na Beach Bay tumalize ratiba ya mechi za mkondo wa kwanza. Matumani yetu ni kuzishinda na kuzoa alama zote sita," alisema.

*Na Hamisi Ngowa*

KATHIANI

### Ukambani kuanzisha kambi

**WANARIADHA** chipukizi kutoka Ukambani huenda wakapata afueni na mkondo mpya wa ufanisi ikiwa mpango wa kuanzisha kambi mpya katika eneo la Iveti utafaulu. Mdhamini mkuu wa mbio za Great Solo Marathon, Sammy Munde Soo alisema kwamba akishirikiana na washirika wake kispoti na wadau wengine, wataasisi kambi ya ukufunzi wa riadha eneo hilo baada ya janga la covid-19 kuisha kwa lengo la kukuza na kustawisha talanta za wanaspoti husika.

*Na Cornelius Mutisya*

KWALE

### Magwiji mbioni kukweza soka

**WALIOKUWA** magwiji wa soka katika wadi ya Mwereni eneobunge la Lunga Lunga, wameanzisha mikakati ya kuimarisha hali ya mchezo huo. Beki wa zamani wa Vijana Sports FC ya mtaa wa Mwena, Thomas Kumbe anaongoza mikakati hiyo kupitia njia ya mtandao wa WhatsApp ambapo wadau wa soka wa eneo hilo wanawasiliana ili kuandaa mikakati ya kurejesha hadhi ya soka eneo hilo baada ya kuisha kwa janga la corona.

*Na Hamisi Ngowa*

Nation Media Group "Digital Copy"

TAIFA LEO

# spoti

TUZO ISIAMULIWE KIHOLELA, AGWANDA AONYA - UK15



MSHAMBULIAJI wa Juventus Paulo Dybala akisherehekea kufunga bao katika mechi ya Serie A mapema Machi. Timu za ligi hiyo zimepewa tarehe ya kurejelea mazoezi katika ishara inayoonyesha uhondo wa spoti utarudi hivi karibuni. *Picha/Maktaba*

# RAHA YAJA

**TURIN, ITALIA**

WANASOKA wa Ligi Kuu ya Italia (Serie A) wametakiwa kurejea kambini mnamo Mei 4 kabla ya vikosi vyote vinavyoshiriki kipute hicho kuanza kujifua kwa michuano iliyosalia msimu huu kufikia Mei 18, 2020.

Haya ni kwa mujibu wa Waziri Mkuu wa Italia, Giuseppe Conte, ambaye amekariri kuwa "hiyo ni mojawapo ya hatua za awali kabisa zitakazorejesha ukawaida nchini humo kadri wanavyozidi kudhibiti maambukizi zaidi ya virusi vya corona".

Katika taarifa iliyotolewa jana na Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), kivumbi cha Serie A kimepangiwa kuanza upya wakati wowote kati ya Mei 27 na Juni 2, huku kikitakiwa kutamatika rasmi kufikia mwanzo wa wiki ya kwanza ya Agosti 2020. Mechi hizo zilizosalia muhula huu zitasakatwa ndani ya viwanja vitupu.

Italia ndiyo nchi ambayo imeathiriwa zaidi na virusi vya corona miongoni mwa mataifa yote ya bara Ulaya. Kufikia jana, zaidi ya vifo 26,600 vilikuwa vimeripotiwa nchini humo. Vifo 260 vilivyotokea mnamo Jumapili ndiyo idadi ndogo zaidi ya watu kuwahi kuaga dunia kutokana na corona nchini Italia tangu Machi 14, 2020.

"Wachezaji wataanza kujifanyia mazoezi kivyao mnamo Mei 4 kabla ya kushiriki mazoezi hayo katika vikundi kunazia Mei 18. Tutatathmini hali itakavyokuwa wakati huo na kuamua iwapo kipute cha Serie A kitarejelewa sasa wiki moja baadaye ili kikamilike mnamo Agosti 2," akatanguliza Conte.

"Muhimu zaidi kwa sasa ni kushauriana mara kwa mara kuhusu namna tutakavyofanikisha mipango hiyo huku tukiendelea kuzingatia kanuni za afya na kudumisha usalama wa wadau wote. Michezo ni sekta muhimu zaidi katika maendeleo yetu kiuchumi," akaongeza.

FIGC tayari imetoa utaratibu utakaoshuhudia wachezaji, makocha, maafisa na wafanyakazi wote katika vikosi vya Serie A wakifanyiwa vipimo vya afya kuanzia Mei 1, 2020.

Mpangilio huo umeigwa na vinara wa FIGC kutoka Ligi Kuu nchini Ujerumani.

**DORTMUND, UJERUMANI**

## Saka sasa windo la Dortmund

BORUSSIA Dortmund wamefichua azma ya kumfanya chipukizi matata wa Arsenal, Bukayo Saka, 18, kuwa kizibo cha Jadon Sancho anayehusishwa na uwezekano mkubwa wa kujiunga na Manchester United mwishoni mwa msimu huu.

Akijivunia jumla ya mabao 17 na kuchangia mengine 19 hadi kufikia sasa muhula huu, Sancho, 20, amekuwa kivutio kikubwa kambini mwa vikosi mbalimbali katika soka ya bara Ulaya.

Mbali na Man-United ambao wako radhi kuweka mezani kima cha Sh17 bilioni kwa minajili yake, klabu nyinginezo zinazokeshea huduma za kiungo huyo mzawa wa Uingereza ni Liverpool, Juventus, Real Madrid na Bayern Munich.

Iwapo Dortmund watashawishika kumwachilia Sancho, kikosi hicho cha Ligi Kuu ya Ujerumani (Bundesliga) kimeweka Saka kileleni mwa orodha ya wanasoka watakaomrithi.

Ingawa kwa sasa anachezeshwa kama beki wa kushoto kambini mwa Arsenal, Saka hutamba sana kila anapowajibishwa katika safu ya kati uwanjani.

Alipangwa katika kikosi cha kwanza cha Arsenal kwa mara ya kwanza mwaka jana katika kivumbi cha Europa League chini ya kocha Unai Emery aliyetimuliwa mwishoni mwa 2019.

Baada ya kuridhisha zaidi katika kibarua chake cha kwanza, Saka alipata uhakika wa kuunga kikosi cha kwanza cha Arsenal baada ya mabeki Kieran Tierney na Sead Kolasinac kupata majeraha yaliyowaweka nje kwa muda mrefu.

Hadi msimu huu wa kivumbi cha Ligi Kuu ya Uingereza (EPL) ulipositishwa kwa muda mwanzoni mwa Machi 2020, Saka alikuwa amewafungia Arsenal mabao matatu na kuchangia mengine manane katika mashindano yote.

Ingawa ni matamanio ya kocha Mikel Arteta kuendelea kujivunia maarifa ya Saka uwanjani Emirates, huenda ikamwia vigumu kumdhibiti chipukizi huyo ambaye gazeti la *The Sun* limesisitiza kwamba atakuwa radhi kupokea mamilioni ya Dortmund badala ya Sh420,000 pekee ambazo kwa sasa analipwa kwa wiki uwanjani Emirates.

## Aston Villa warai wachezaji wao wakubali kukatwa posho

**LONDON, UINGEREZA**

SIKU chache baada ya wanasoka wa Arsenal kukubali kukatwa asilimia 12.5 ya mishahara yao, Aston Villa sasa wametaka wasimamizi wakuu pamoja na wachezaji wao kunyofolewa asilimia 25 ya malipo yao ya kila mwezi kwa kipindi cha miezi minne ijayo ili kukabiliana na janga la corona.

Wakati uo huo, Norwich City wametetea hatua yao ya kupunguza mishahara ya vibarua na wafanyakazi wao wengine ambao si wachezaji kwa kufichua kwamba huenda wakapoteza zaidi ya Sh4.9 bilioni kutokana na virusi vya corona.

"Maamuzi tuliyofanya ni kwa minajili ya mustakabali wa klabu na maslahi ya wafanyakazi wetu wote," akasema Afisa Mkuu Mtendaji wa Norwich, Ben Kensell.

"Huwa tunajikusanyia mapato ya hadi Sh17 bilioni kwa mwaka. Kati ya hizo, Sh13 bilioni hutokana na matangazo ya kibiashara na upeperushaji wa moja kwa moja wa mechi zetu runingani. Tayari tumetumia zaidi ya Sh18 bilioni msimu huu, hivyo tumeanza kukadiria hasara ya Sh1 bilioni," akasema Kensell.

Hadi kivumbi cha EPL kiliposimamishwa mwanzoni mwa Machi 2020, Norwich walikuwa wakikokota nanga mkiani mwa jedwali kwa alama 21, nne nyuma ya Aston Villa na sita zaidi nyuma ya Bournemouth ambao pia wako katika hatari ya kuteremshwa daraja. Newcastle United na Norwich City ndizo klabu za kwanza za Ligi Kuu ya Uingereza (EPL) kupunguzia wafanyakazi wao wasio wachezaji malipo ya kila mwezi.

Taifa Leo - Jumanne

6 161105 100119

Ukiwa na suala lolote ungetaka kuwasilisha kwetu, tuma sms bila malipo kwa **20684** ukianza na neno 'Taifa'

Hutayarishwa katika Nation Centre, Kimathi Street, na kuchapishwa Mombasa Road, Nairobi, na kampuni ya Nation Media Group, S.L.P. 49010, GPO Nairobi 00100, Simu: 3288000, 0719038000, Fax: 2213946. Ime orodheshwa katika Posta Kuu kama Gazeti.

Nation Media Group "Digital Copy"